
# Msalaba Uliotahiniwa Na Msalaba Ulioshuhudiwa



Adrian Ebens

# Msalaba Uliotahiniwa
# na
# Msalaba Ulioshuhudiwa

*Athari na maana ya Msalaba wa Kristo*

Ari kwa rafiki zangu wapendwa

Tor na Azadeh

Kimechapishwa na

fatheroflove.info

maranathamedia-kenya.com

© Adrian Ebens, 2019

adrian@life-matters.org

# Yaliyomo


1. Baba Wasamehe ..................................................................................... 4

2. Msulubishe! .......................................................................................... 10

3. Katika Mateso Yao Yote Yeye Aliteswa.................................................... 14

4. Hamkuweza Kukesha Pamoja Nami Kwa Saa Moja? ................................ 20

5. Dhabihu na Matoleo Hukupendezwa Nazo ............................................. 24

6. Sisi Tunayo Sheria ................................................................................... 34

7. Kama vile Musa alivyomwinua yule Nyoka kule Jangwani ....................... 47

8. Ee Mungu Njia yako i katika Patakatifu .................................................. 53

9. Sela......................................................................................................... 62

# 1. Baba Wasamehe

Taswira ilijengeka akilini mwangu ikichochea mawazo ya ndani ya kujuta. Katalogi iliyokuwa ikikua ya kumbukumbu za mwingiliano wangu wa wasiwasi na wale ambao walinizunguka zilikuwa zinakuwa mzigo kwa nafsi yangu. Utafutaji wangu wa amani sasa ulikuwa mkuu. Nilipoangazia milipuko yangu ya hivi karibuni nilihisi haja ya kujikana nafsi na hamu ya kuwa mtu tofauti na yule ambaye nilijitambua kuwa kwa wakati huo. Neno ambalo lilitawala mawazoni mwangu wakati huo lilikuwa *msamaha* na hitaji langu la msamaha.

Katika maisha yako umewahi fikia katika kiwango ambacho unatambua kuwa mtu uliye sio mtu ambaye unapenda, na hata baada ya majaribio mengi ya kubadilika, unafika pahali pale pale na mzigo wa hisia zilezile? Unawezaje kuepuka taswira hiyo ya kusumbua unayoiona ndani yako?

Hisia hii inathibitisha ukweli wa Neno la Bibilia.

> …Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja. (11) Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu, hakuna hata mmoja amtafutaye Mungu. (12) Wote wamegeukia mbali, wote kwa pamoja hawafai, hakuna atendaye mema, naam, hata mmoja. Warumi 3:10-12

Kuna wengi ambao wanatafuta kuepuka hali hii kwa kujipofusha kuhusu dosari ya tabia zao wenyewe na kuangazia hatia za wengine. Kwa vile sisi sote tuna dosari katika tabia ni rahisi kupata kitu cha kumlaumu mwingine kwa sababu ya hali ngumu ambazo tunaweza jipata ndani yake. Kutafuta kupata amani kwa njia hii ya kuepukika itaharibu mahusiano tuliyonayo na wengine na hatimaye kutusababishia hata huzuni na upweke mwingi.

Njia pekee ya amani na uhuru ni kuwajibikia mambo yetu wenyewe na kutafuta msamaha kutoka kwa Muumbaji wetu.

> Ndipo akaanza kuwafundisha, akisema: (3) “Wana heri walio masikini wa roho, maana hao Ufalme wa Mbinguni ni wao. (4)

> Wana heri wale wanaohuzunika, maana hao watafarijiwa. Mathayo 5:2-4

Ni katika hali hii haswa nilijipata. Nilikuwa nikiombolezea ubinafsi wangu na uchungu niliowatia wengine kupitia kwa hitaji langu la kutaka kupewa makini.

Nililelewa katika nyumba ya Kikristo na nilikuwa nimefunzwa kuhusu upendo wa Mungu kama ulivyodhihirishwa katika Yesu Kristo. Nikiwa mtoto nilisikia maneno haya yakinenwa mara kadhaa:

> Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Mathayo 11:28

Nilitiwa wazo kuwa naweza mwendea Yesu ili kupata pumziko na kupumzishwa kutoka kwenye mzigo wangu. Nilianza kuyaangazia maisha ya Kristo na hasa mazingira ya mwisho yanayohusiana na kifo chake. Kisa cha Msalaba kina nguvu nyingi kwa nafsi ambayo imevunjika na kufika mwisho wa uwezo wa kujiokoa. Msalaba umebadilisha maisha ya mamilioni na kuwapa amani na tumaini. Lakini bado uko na after. Ni jinsi gani kisa cha usaliti, kuteswa na kuuawa kwa mtu mwenye haki miaka 2000 iliyopita kinaweza leta amani kwa nafsi? Hili linafaa vipi kwangu hivi leo?

Mwanzoni, kisa hiki kinahisika kama kabiliano-angavu. Si haiwezi kuleta maana zaidi kuingia katika sehemu ya utulivu iliyojawa na harufu nzuri ya kupendeza na muziki wa amani ukizingirwa na urembo halisia kuleta amani kama hiyo? Kisa cha Msalaba kinapokuwa hai katika nafsi, tunasikia sauti za askari zikiguruma, mpasuko mkubwa wa viboko juu ya mgongo wa Kristo, mlio wa kuuguza wa msalaba mkubwa wa mbao ukianguka sakafuni Mkombozi akizimia chini ya uzito wake. Tunasikia kebehi za umati na nyuso za mashahidi zilizokunjama kwa ukatili kufurahia katika mazingira ya unyama.

Ni siri gani iliyoko katika after hii? Kisa hiki kinawezaje nipa amani? Kunawezaje kuwa na utulivu unaotokana na mauaji?

Kuna hamu yenye uwezo wa kugeuza mbali kutazama kwa mtu kutoka kwa eneo na ila kuna nguvu hizi za mvuto ambazo hukuwasia kutazama mchezo huu wa kuigiza. Kwa namna fulani ukatili wake unafahamika wa ajabu na kwa wakati uo huo wa kutisha. Tunafika katika pahali pa fuvu – Golgotha. Yesu kwa upole analala juu ya kifaa hiki cha mateso; damu ilikuwa ikitiririka kutoka kwa uso wake kwa sababu ya taji ya maskhara iliyoundwa kwa miiba iliyokuwa imegongelewa kichwani mwake na umati. Watu walikuwa wakiteseka hatma hii pamoja naye walipinga mno, wakitafuta kuchelewesha kuepukika. Mgongo wa Mkombozi hautambuliki kutokana na viboko alivyokuwa amepigwa awali. Lakini mtu huyu ametenda nini kustahili hayo?

Usomaji mdogo wa kisa cha Injili unadhihirisha uzima ulijawa na huruma, wema na sura ya kupendeza sana ya Baba yake aliye mbinguni aliyejawa upendo na wema. Inawezekanaje kwamba mtu huyu anaweza tendewa ushenzi kama huu?

Mkwaruzo mkubwa wa chuma huteka makini yetu kadri mwiba unatiwa kupitia kwa mikono hiyo tefu ambayo ilikuwa imewabariki wengi. Miguu hiyo ya thamani ambayo ilikuwa imetembea kwenye barabara za mchanga za Israeli sasa ilikuwa imedungwa na kutundikwa kwa msalaba wa mbao. Kisha msalaba unainuliwa juu na kutiwa kwa ukali katika pahali pake ili ulimwengu wote uushuhudie, kwa sababu tukio hili liliacha rekodi katika Maandiko lielezewe na kusomwa na mamillioni kwanzia hatua hiyo kuendelea.

Nilipotafakari tukio hili la msalaba katika kutafuta ondoleo la hatia yangu, moyo wangu ulijawa na huruma kwa mtu huyu asiyekuwa na hatia ambaye pia ni Mwana wa Mungu. Mawazo yangu yalifuata chanzo cha nyayo zake kutoka Gethsemane hadi Kalvari. Nilitafakari maneno ya Pilato gavana wa Kirumi:

Tazameni, huyu hapa huyo mtu. John 19:5

Nilimtazama akiyumbayumba na kuanguka katika bustani na kutiririkwa na jasho la matone ya damu katika uchungu mwingi. Nilitazama wanafunzi wake wakikimbia na kumuacha kwa rehema ya umati. Nilistaajabu kwa mshangao jinsi umati ungemchagua Baraba na kutaka kumsulubisha Mwana wa Mungu. Mbona wanafanya hivi? Ni uovu upi ametekeleza ili kustahili hili? Nilitazama alipokuwa akidhihakiwa, kupigwa na kutusiwa:

> Wakamvua nguo Zake na kumvika vazi la rangi nyekundu, kisha (29) wakasokota taji ya miiba wakaiweka kichwani pake. Wakamwekea fimbo katika mkono wake wa kuume, wakapiga magoti mbele zake na kumdhihaki wakisema "Salaam, mfalme wa Wayahudi!'' (30) Wakamtemea mate, wakachukua ile fimbo wakampiga kichwani tena na tena. (31) Baada ya kumdhihaki, wakamvua lile vazi, wakamvika tena nguo Zake. Kisha wakampeleka ili kumsulibisha. Mathayo 27:28-31

Jaribu la kuwalaumu watendaji unyama katika drama hii lilikuwa lenye uwezo lakini wakati huo niliwaza kuhusu unyama nilioutenda kwa wengine na nikatambua kwamba nilikuwa na hatia kama wao tu. Maneno ya Kristo yaliniingia mawazoni:

> …Amin, amin ninawaambia, kwa jinsi mlimvyotendea mmojawapo wa hawa ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi. Mathayo 25:40

Kwani sikuwa nimewacheka na kuwadhihaki wengine? Sikuwa nimetazama sinema zinazoonyesha ukatili na kufurahia wakati wale ambao nilifahamu kuwa wapumbavu wakikutana na kifo chao? Sikutoa maneno ya laana midomoni mwangu dhidi ya wale niliowaona walikuwa wamenikosea? Hisia zangu za hukumu ziliongezeka niliposoma. Nilipowazia kuhusu watu wawili waliokufa pamoja na Yesu nilijitambulisha na maneno ya mtu aliyesema:

> Sisi tumehukumiwa kwa haki kwa kuwa tunapata tunayostahili kwa ajili ya matendo yetu. Lakini huyu mtu hajafanya kosa lo lote." Luka 23:41

Hukumu niliyokuwa nimeikusanya kwa wengine ambao walikuwa wakinizuia na kunisumbua awali sasa walikuja nyumbani kwa nguvu nilipokuwa nikimtazama Kristo msalabani. Nilihisi athari za maneno:

> Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea. Mathayo 7:2

Katika kipindi cha milele nilistajabishwa na kutazama juu ya Msalaba. Ingawa halisia miaka 2000 baada ya tukio hili, nilijihisi binafsi kuwa pale kama shahidi wa drama hiyo. Ulimwengu wangu uliingia katika mwendo wa kujikokota na kelele na vurugu iliyozunguka msalaba ilitulia nilipokuwa nikimtazma Mwana wa Mungu na kujifunza kwamba uso mzuri maneno hutoka katika midomo yake

> “Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo" Luka 23:34

Umuhimu wa maneno ulipopenyeza rohoni mwangu, cheche ya tumaini huzalishwa ndani. Msamaha uliotamaniwa kwa muda mrefu na kutumainiwa unajiwasilisha mbele yangu kwa ufasaha. Nilipopiga magoti mbele ya muumba wangu na machozi yakitiririka mashavuni mwangu, nilitazama katika uso wa upendo na moyo wangu uliyeyuka. Katika uso huo hakukuwa hata nyuzi moja ya hukumu. Nilikuwa na hisia nzito za uhalisia kwamba maisha yangu ya uovu yalikuwa sehemu ya sababu alikuwa akiteseka msalabani na ila hapakuwa na hukumu kutoka kwake – upendo na msamaha pekee.

Hakunilaumu kwa sababu ya mateso niliyomsababishia. Alinisamehe bure tu. Swali lilikuwepo na bado lipo, je nitaukubali? Nitaamini kwamba nimesamehewa? Kwa upande wangu niliupokea kwa mikono yangu miwili na kudai urithi wangu wa uzima wa milele. Nilimwambia Yesu pole kwa yale ambayo nilikuwa nimetenda na kumuomba awe Bwana wa maisha yangu. Mara moja amani hii ilikuja juu yangu, ndivyo uponyaji, ndivyo kutuliza, na ndivyo kukomboa. Mzigo wa hatia uliokuwa ukinivunja ulitoweka na nilihisi furaha rohoni mwangu ambayo haiwezi elezeka bali kushuhudiwa na wale ambao wanaikumbatia.

Kama chemchemi ya maji ya uzima, maji yalimwagika kutoka machoni mwangu kwa shukurani. Mengine niliyokuwa nikitafuta hatimaye yalikuwa yangu. Shukurani niliyohisi ilikuwa nyingi na kwa furaha nikaitiisha kwa uongozi wa Mkombozi wangu.

Ndivyo ilivyokuwa na ndivyo ilivyo ushuhuda wangu mzuri na uliyobarikiwa na Msalaba. Unazua maswali mengi. Ni jinsi gani kitu kizuri kinaweza jitokeza kwa kitu cha kutisha? Ni jinsi gani tukio hili ambalo lilitendeka miaka 2000 iliyopita linahisika kana kwamba limetendeka leo? Ni mambo yepi muhimu ambayo yalileta hili na mbona ujali kuhusu swali hili la Msalaba na kushuhudia kwako binafsi? Wacha tuutahini Msalaba tuone.

## 2. Msulubishe!

> …Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa viongozi wa makuhani na walimu wa sheria, nao watamhukumu kifo (19) na kumtia mikononi mwa watu Mataifa ili wamdhihaki na kumpiga mijeledi na kumsulibisha... Mathayo 20:18-19

Mbona viongozi wa Israeli walimchukia Yesu hivyo sana? Mbona walidhamiria sana kumwangamiza? Ni jinsi gani mtu ambaye alileta fahari na furaha ulimwenguni kuwa tishio?

> Nuru halisi, imwangaziayo kila mtu ilikuwa inakuja ulimwenguni. (10) Alikuwepo ulimwenguni na ingawa ulimwengu uliumbwa kwa Yeye, haukumtambua. (11) Alikuja kwa walio Wake, lakini wao hawakumpokea. Yohana 1:9-11

Viongozi hawa walikuwa wawakilishi wa jamii yote ya mwanadamu katika hali yao asili na tabia yao kwa Mwana wa Mungu mteule wa Baba.

> Maana alikua mbele zake kama mche mwororo, Na kama mzizi katika nchi kavu; Yeye hana umbo wala uzuri; Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani. (3) **Alidharauliwa na kukataliwa na watu**; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, **Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu**. Isaya 53:2-3

> Wafalme wa dunia wanajipanga, Na wakuu wanafanya shauri pamoja, Juu ya Bwana, Na juu ya masihi wake. (3) Na tuvipasue vifungo vyao, Na kuzitupia mbali nasi kamba zao. Zaburi 2:2-3

Kisa cha Msalaba ni kipindi wazi kabisa katika historia ya mwanadamu kikidhihirisha tabia yetu kwa jumla kwa Mwana wa Mungu katika urithi wetu asili kutoka kwa Adamu. Kisa hiki kinathibitisha ukweli wa kauli ya Paulo aliposema:

> Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Warumi 8:7

Ukatili huu ulitoka wapi? Hapo mwanzo kabisa Mungu alikuwa amewaagiza Adamu na Hawa kwamba kulikuwa na mti katikati ya bustani ambao hawakupaswa kula matunda yake. Kula kutoka kwa mti huu kungepelekea kufa kwao na watakoma kuwepo. Mti uliwekwa katika bustani ili kuwapa Adamu na Hawa fursa ya kuchagua kumtumikia muumba wao. Bila uwepo wa kanuni hii katika bustani hawangekuwa na uwezo wa kuufanyisha zoezi uchaguzi wao. Ila kuchagua kinyume cha Mungu ni kujitenga kutoka kwa chanzo cha uzima.

Ni namna gani maneno ya Mungu yanaweza eleweka? Yalitolewa kwa upendo usio na mwisho na utunzaji wa ustawi wa Adamu na Hawa? Shetani akichukua nafasi yake kupiga kupitia kwa mtindo wa nyoka aliweza kupendekeza nia tofauti kwa Hawa ya mbona Mungu alikuwa amesema hili.

> Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, (5) kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. Mwanzo 3:4-5

Shetani anadokeza kuwa Mungu ni mbinafsi na anatafuta kuwazuia Adamu na Hawa wasifikie uwezo wao wote. Kuweka nia hii kwa maneno ya Mungu kunabadilisha kikamilifu maana ya kile Mungu alisema kama wangekula tunda hilo. Shetani anaelezea madai yake kwa mantiki mgeuko. "Hakika hamtakufa." Hili linapendekeza kwamba Mungu angehakikisha kwamba wamekufa kwa sababu inavyoonekana alikuwa na nia binafsi ya kuzuia uwezo wao wote. Hili linamaanisha kwamba Adamu na Hawa walielewa kwamba *lazima watakufa* badala ya *watakufa*. Kwa njia nyingine, walifahamu kwamba Mungu angewaweka katika Kifo badala ya Mungu angeruhusu wajiangamize katika maovu yao. Tofauti ni kubwa.

Adamu alichukua na kula tunda akiwa katika hisia kwamba Mungu angemuua mke wake kwa sababu ya uasi wake. Katika dhana hii kwamba Mungu alikuwa muuaji, Adamu aliamua katika roho ya chuki na uasi

kumpinga Mungu na kusimama na Hawa katika chochote kitakachomfanyikia. Kwa wakati uo huo pia alishanga kama maneno ya nyoka yalikuwa kweli na hili lilimtia moyo kuchukua tunda na kujiunga na nyoka katika kumuasi Mungu.

Hapa tunapata chanzo cha chuki ya mwanadamu kwa Mungu. Alikuwa na wazo lisilosawa la tabia yake na alitenda kwa uongozi wa wazo hilo. Kwa kuamini kwamba Mungu angelinda maslahi yake mwenyewe kupitia kwa kuwaua wengine, Adamu aliweka wazi tabia hii alipohofia juu ya uzima wake kupitia kwa kuswali.

> Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. (11) Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? (12) Adamu akasema, **Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala.** Mwanzo 3:10-12

Adamu alihofu kwa sababu alikuwa chini ya wazo la uongo kwamba Mungu alikuwa amekuja kumuua. Anapoulizwa kama amekula tunda la mti ambao aliagizwa asile alielekeza lawama kwa mke wake na kwa Mungu. Kiasili adamu alikuwa akisema "kama yeyote atakufa basi unapaswa kumchukua mke wangu na umuue na pia unapaswa kuuawa kwa sababu ulimuumba!"

Yote haya yanatokea kwa dhana ya uongo kwamba Mungu angeua ili kulinda maslahi yake. Kama alivyojua hakuna njia ya kujiondoa kuliko mtu kuuawa, anamhukumia mke wake na Mungu kifo ili kulinda maslahi yake. Tunagundua kwa mvuto kwamba mawasiliano yote na mwanadamu baada ya anguko yalipitishwa kwa Mwana wa Mungu ambaye ndiye mpatanishi mmoja kati ya Mungu na watu. 1 Tim 2:5. Hivyo Adamu alimhukumu mwana wa Mungu kifo kwa kumuumba mwanamke ambaye angemjaribu kuvunja amri ya Mungu. Katika maneno hayo "mwanamke uliyenipa awe pamoja nami" yako na mbegu ya kilio "msulubishe" ambayo yangeibuka miaka 400 baadaye.

Mbegu hii ilikaa ndani ya moyo wa Adamu na uhalisia huu ulikuwa umefichwa kutoka hata kwake yeye mwenyewe. Kama Mwana wa Mungu angekabiliana na Adamu katika shtaka kuwa ulikuwa mpango wa Adamu kumuua Kristo, angejibu kwa namna ambayo uzao wake ulifanya.

> … Kwa nini mnataka kuniua? Ule umati wa watu ukamjibu, "Wewe una pepo mchafu! Ni nani anayetaka kukuua? Yohana 7:19,20

Adamu angekataa mashtaka ya Mwana wa Mungu kama mwitikio zaidi pengine tatizo ndogo. Njia pekee ya kuondoa mbegu hii ya kifo ilikuwa iwekwe wazi kisha kwa Adamu kutubu maovu yake kwa Mwana wa Mungu.

Mbegu hii ya mauti ni urithi wa kila mwanamume na mwanamke. Hila na bila kuoneka tuna uasi huu asilia kumwelekea Mungu na hamu ya kumuumiza Mwanawe. Hiyo ndio sababu anadharauliwa na kukataliwa na watu wote sio tu na watu ambao walimsulubisha kihalisi miaka 2000 iliyopita.

Maana ya hili inafika mbali na kwa hivyo kanuni ya Msalaba haijawekewa siku moja tu katika historia ya mwanadamu lakini badala yake inapanuliwa katika kila siku ya historia ya mwanadamu.

## 3. Katika Mateso Yao Yote Yeye Aliteswa

> Nao watu wote waishio duniani watamwabudu huyo mnyama, yaani, wale wote ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kitabu cha uzima cha **Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu.** Ufunuo 13:8

Yesu aliponena juu ya Msalaba alifanya hivyo kwa istilahi pana zaidi kuliko vile watu wengi wanaweza tambua.

> Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Mtu ye yote akitaka kunifuata, ni lazima **ajikane mwenyewe na auchukue msalaba wake**, anifuate. Mathayo 16:24

Kanuni ya Msalaba ni moja ya kujikana nafsi. Yesu alionyesha hili katika matukio yaliyopelekea kusulubishwa kwake. Hakujikinga dhidi ya kejeli na kichapo alichopokea. Aliziinamia kwa uvumilivu hata ingawa zilimsababishia mateso makubwa. Nguvu zote za ulimwengu zilikuwa chini ya amri yake. kwa mara moja angefanya mateso yake kuisha lakini alitii kwayo ili kuwapa wauaji wake muda mrefu iwezekenavyo kubadili mawazo yao kumhusu. Kristo alitumaini kwamba wangetubu matendo yao kabla ya kujiangamiza katika angamizo la Yerusalemu miaka arobaini baadaye.

Uhalisia ni kwamba vitu vyote vimeshikamanishwa pamoja katika ulimwengu huu na Mwana wa Mungu.

> Yeye alikuwapo kabla ya vitu vyote na **katika Yeye vitu vyote vinashikamana pamoja**. Wakolosai 1:17

> Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, **akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza.** Waebrania 1:3

Kama aliyetuumba Kristo kama mzazi tefu anatamaa juu ya kila mwanamume, mwanamke, na mtoto. Anataka kila mmoja wa wana wake kukua katika furaha, afya na mazingira yenye amani. Tamaa yake ni onyesho la Baba yake ambaye ni chanzo cha vitu vyote. Hili humaanisha

kwamba kila wakati mmoja wa wana wake anapitia uchungu, Kristo anapitia uchungu. Moyo wake huuma kwa mateso yote ya mwanadamu. Nabii Isaya alinena kuhusu hili akisema:

> **Katika mateso yao yote yeye aliteswa**, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale. Isaya 63:9

Kila jambo moja ambalo Waisraeli waliteseka kama taifa na kama mtu binafsi, Kristo aliteseka pamoja nao. Lakini sio kwa Waisraeli tu ndio Kristo aliteseka, bali kwa wote ambao wanaishi juu ya dunia.

Kwa wale ambao wako na wana, huwa unahisi aje wakati ambao mtoto wako yuko katika uchungu mwingi? Huchoma moyo wako na hukusababishia mateso mengi na huzuni. Na vipi kama mmoja wa wanao humjeruhi mwingine wa wanao? Hili husababisha hata huzuni mwingi. Unateseka kwa sababu ya mwanao ambaye amejeruhiwa na kuhisi kusikitishwa na yule ambaye amelazimisha jeraha.

Mzazi anahisi aje wakati mtu wa nje ya familia anapomuumiza mwanawe? Hisia asili kwa wengi ni kumwadhibu mtu huyo. Yesu anahisi vipi wakati mmoja wa wanawe amenajisiwa? Hili humsababishia huzuni mwingi kuliko jinsi mzazi mwanadamu anahisi kwa mwanawe. Itikio la mwanadamu la kukabiliana na mhusika ni kumwadhibu. Kwa Kristo mhusika pia ni mwanawe. Hujeruhiwa na matendo yao maovu lakini akiondoa ulinzi wake kutoka kwao watakufa na hataki yeyote afe. Hivyo basi Kristo huteseka kimya wakati waume, wake na watoto huumizana, hunyanyasana na huuana.

Kila wakati tunatenda dhambi, tunapinga wito wa Roho wa Kristo rohoni mwetu. Kila wakati tunatenda kile ambacho tunajua kwamba sio sahihi, tunamchoma Kristo.

**Kisha** wakaanguka, **kwa kuwa kwa nafsi zao wanamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili** na kumfedhehi hadharani. Waebrania 6:6

Kila wakati mtu anapompiga mwenzake kofi, Kristo anahisi. Kila wakati mtoto anapotetemeka kwenye ukuta baba yake anapompiga na kumchapa mamake, Kristo anahisi yote. Lakini hawezi walazimisha kuacha kutenda mambo haya kwa sababu matumizi ya nguvu hayabadilishi tabia ya wale wanaotenda maovu lakini bila shaka itabadilisha tabia ya Mungu kama alitumia nguvu. Lakini Andiko linasema Mungu habadiliki (Malaki 3:6). Pia zingatia kwamba kama mtu atatambua Mungu anawalazimisha, inaweza wafanya hata kuamua kupinga na kutenda maovu zaidi.

Tunapoelewa mateso ya Kristo katika uchungu ambao wanadamu wanauweka juu ya wengine tunapata mtazamo wa Kristo ambao unang'aa sana kwamba haiwezekani kuishi kwa njia ile ile kabla ya utambuzi huu. Zingatia takwimu ifuatayo kutoka kwa *worldometer.info*

Kulingana na WHO, (World Health Organisation) kila mwaka ulimwenguni kuna kadirio la milioni 40-50 la uaviaji mimba. Hili linalingana na takriban 125,000 ya uaviaji mimba kila siku.[1] Ebu tuwaze mateso ambayo Kristo anapitia katika kufa kwa watoto wake 125000 kwa njia hii – kila siku? Na vipi kuhusu hisia kwa mama anapojaribu kukubaliana na kuiavya miimba yake? Hakuna njia akili ya mtu mmoja inaweza fahamu mateso ambayo yanahusika katika takwimu hii.

Leo takriban watu 3000 watakufa katika ajali ya gari na watu 2800 watajitoa uhai wao wenyewe. Ni mateso kiasi gani yanahusishwa katika takwimu hiyo sio kwa wale waliokufa bali kwa wale ambao wanaachwa nyuma? Ni wanawake na watoto wangapi ambao watadhulumiwa kimapenzi leo na wanaume? Takwimu zinaonyesha karibu watu million 25 wanauzwa kama watumwa na zaidi ya nusu yao wanadhulumiwa kimapenzi.[2] 71% ya million

[1] worldometers.info/abortions/

[2] https://www.bustle.com/p/13-sex-trafficking-statistics-that-put-the-worldwide-problem-into-perspective-9930150

25 ni wanawake na wasichana. Leo wanawake 137 watakufa katika mikono ya wenzi wao au wenzi wa awali mahali ulimwenguni.[3] Mateso yanayowekwa juu ya Kristo katika takwimu hizi hayana mfano. Hizi ni takwimu chache tu zinazoakisi mateso ulimwenguni kila siku.

Kila siku Kristo analazimishwa kuvumilia ukatili na ubinafsi wa wanaume na wanawake. Mtu anaweza uliza swali mbona Kristo hawezi jiokoa na ashuke kutoka kwa Msalaba huu wa kujikana nafsi? Kila siku ni jahanamu ya kudumu kwake na malaika wake wapendwa ambao wanatumwa kutulinda na ambao wanashuhudia mauaji haya. Umewahi tamani kuwa ungekuwa malaika? Fikiria kwa makini ni huzuni kiasi gani wamevumilia kwa kuwatunza wana na Binti wa ulimwengu huu walioanguka. Hiyo ni kazi ambayo utaitenda kwa kwa kujitolea? Kulazimishwa kumuona mtoto akinyanyaswa kwa sababu hakuna yeyote anayemuomba Yesu kuwasaidia au wanafunga akili zao kwa mwanga unaotumwa kwao. Ni unyonge na huzuni wa namna gani malaika anayeshuhudia hali kama hiyo atahisi?

Fikiria tatizo la mzazi wa binti aliyetawaliwa na dawa za kulevya katika uhusiano wa vurugu na mume mnyanyasaji. Utafanyaje kukomesha? Utamlazimisha binti yako kubadilika? Utauma vidole vyako na kuuacha uchungu wote utoweke? Na je, binti yako akikataa kusaidiwa, unaweza wafanya wabadilike? Bila wao kukubali, unaweza fanya machache isipokuwa kutembea kwalo pamoja nao ukiwaambia kwamba unawapenda na kufanya kila uwezalo kuwafariji wanapotembea kwenye bonde lao la giza. Kujaribu kuwalazimisha wabadilike ni kuwaingiza ndani zaidi tu kwa tatizo lao.

Baba yetu na Mkombozi wako katika hali sawa, ingawa wako na rasilimali isiyo na kikomo, hawawezi lazimisha mapenzi ya watoto wao na hawawezi tufanya tubadilike isipokuwa tuombe msaada wao na kusikiliza uongozi wao na kuufuata.

---

[3] BBC.com The Women killed in one day around the world. 28th Nov 2018

Kwa mawazo ya mwanadamu, Msalaba unaonekana kutowezekana kuuamini kwa sababu ni tofauti kabisa na tunavyofikiria. Hakuna kujitetea, kuhifadhi nafsi au mapenzi ya mtu binafsi. Ni kujikana nafsi kikamilifu kwa huduma, kufariji na msaada wa watoto wako wengi ambao hawataki chochote kinachohusiana nawe.

Kuna watu wengi ambao wamemkasirikia Mungu kwa sababu anaonekana kutojali kuhusu mateso yao. Ila watu wanapokataa kumtambua au kutunza amri zake, anawezaje kumzuia Shetani asiwavamie wakati wanampa ruhusa kuharibu maisha yao kupitia kwa kukataa kwao kutembea katika njia za Mungu?

Kwa wale ambao tunaamini ndani ya Mungu na kutafuta kufuata njia zake, unaweza ona kwamba Msalaba wa Kristo sio tukio la siku moja bali uzoefu ambao unajumuisha historia yote ya mwanadamu? Ni ukweli kwamba Kristo alikufa mara moja katika mwili lakini tukio hili ni ufunguo wa kutufungulia ukweli kwamba Kristo anachomwa kila siku na mawazo ya watu, maneno na matendo. Zingatia fungu lifuatalo la Bibilia

> **Nimesulibiwa pamoja na Kristo**, wala si mimi tena ninayeishi bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu. Wagalatia 2:20

Mbona Paulo anasema kwamba amesulubiwa *pamoja na* Kristo, mbona hasemi nimesulubiwa kama Kristo? Kama nimesulubiwa *pamoja na* Kristo basi hili halipendekezi kwamba Kristo bado anasulubiwa kupitia uovu wa watu hivi leo?

> Twateswa lakini hatuachwi, twatupwa chini lakini hatupondwi. (10) **Sikuzote twachukua katika mwili kufa Kwake Yesu** ili kwamba uzima wa Yesu uweze kudhihirika katika miili yetu. 2 Wakorintho 4:9-10

Mbona Paulo anazungumzia kuchukua katika miili yetu kufa kwa Bwana Yesu? Imeandikwa kwa wakati uliopo sio uliopita. Hili halioneshi kwamba

katika mateso na kuteseka kwa wale ambao wanamfuata Kristo, kwamba Kristo huteseka pamoja nao na anaguzwa na huzuni na uchungu wao?

Basi uitikio wa mwanadamu ni upi kwa Msalaba huu? Ni vigumu kujiishia kama unawaza kuhusu mateso yake kila siku. Unawezaje ishi kujitukuza ukijua kwamba Kristo yuko katika sumbuko na uchungu mwingi kila siku?

Siku moja nilipokuwa nikitafakari kuhusu suala hili na kuhisi kulemewa kabisa na mateso yake nilimwagiza kwa maombi "naweza kuaje mbaraka kwako na kukusaidia kwa mwanga wa mambo haya?" Jibu lilikuwa "unaweza kesha nami kwa saa moja?" msomaji mpendwa, nakukaribisha utafakari juu ya kuteseka kwa mkombozi wetu. Vitu vya maisha haya unavyotafuta kufurahia ambavyo unajua vinakuzuia kutembea karibu zaidi na mkombozi wako vinastahili mateso ambayo Mkombozi wetu anahisi? Kwa kila sekunde ulimwengu huu unaendelea katika hali yake ya sasa Kristo huvumilia uchungu ambao hauwezi elezeka. Kila pumzi unayopumua ni ya thamani isio kadiriwa kwa sababu ya mateso ambayo imemgharimu Mwana wa Mungu. Moyo wake wa huruma daima hautalazimisha watu kubadilika bali husubiri kwa hamu tuje kwake ili tupate pumziko.

Mungu hatufanyi kuwajibikia mateso yote ya ulimwengu na hatuwezi badilisha ulimwengu wote kwake kwa uwezo wetu bali kwa kuaza kila siku kwa kujikana nafsi kwa Kristo na kiwango cha upendo na uvumilivu anaotuonyesha kupitia kwa uchungu na kujikana nafsi, tunaweza badilishwa kuwa wavumilivu kwa wengine na kukaa na makosa yao na udhaifu wao bila hitaji la kulalamika au kuwashwa.

Kizazi kisichokuwa na kikoma cha milele hakiwezi kamwe eleza urefu na upana wa mateso ya Msalaba miaka hii elfu sita iliyopita. Kujikana nafsi kunakoonyeshwa kunaweka wazi kabisa ubinafsi wetu asili. Kuwaza msalaba kwa njia hii hukufanya kunyenyekea kwa upole au kuwa mgumu na kupinga na kupigana dhidi ya ufunuo kama huo wa ndani wa upendo wa Mungu.

Utaruhusu nafsi yako kuvutwa kwa upendo wa Mungu katika udhihirisho huu wa Msalaba na kuzingatia kuwa Kristo amechinjwa katika Roho wake kwanzia kuwekwa msingi wa ulimwengu hadi sasa? Isingekuwa ni kwa ufunuo wa Msalaba halisi hatungejua hisia zetu asili kwa Kristo. Katika kifo cha Kristo miaka 2000 iliyopita, mbegu ya uadui ndani ya Adamu ilidhihirishwa kikamilifu na binadamu aliona matokeo kamili ya kile kilikuwa moyoni mwa Adamu bila kukuzwa wala kufahamika.

Sasa vile tunaufahamu wa Msalaba huu, tutauitikiaje?

## 4. Hamkuweza Kukesha Pamoja Nami Kwa Saa Moja?

Kisa cha Msalaba wa Kristo kina kabiliana na yeyote ambaye bado anasalia na mawazo ya hisia katika ubinadamu wao. Kwa roho masikini ambazo zimeichukua kazi ya kuwaua wanyama na watu, unyeti kama huo unawekwa kwa kiwango hatari.

Wakati wanafunzi walimtazama Masihi wao akisimama mbele ya watu na kunena kwa uwezo na ushawishi wa ufalme wa Mungu, walijivunia kuhusishwa naye. Kilikuwa kisa tofauti alipokuwa akibeba msalaba njiani Kalvari. Udhalilishaji na kifo cha Msalaba ni kitu ambacho uasili wa binadamu haupendi kuhusishwa nao. Hili liliwekwa wazi katika maisha ya Petro ifuatavyo:

> Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaeleza wanafunzi wake kwamba hana budi kwenda Yerusalemu na kupata mateso mengi kwa mikono ya wazee, wakuu wa makuhani na walimu wa sheria na kwamba itampasa auawe na siku ya tatu atafufulika. (22) **Petro akamchukua kando akaanza kumkemea, akisema, "Mungu apishie hayo mbali**! Jambo hili kamwe halitakupata!!'' Mathayo 16:21-22

Petro hakumtaka Yesu anene kuhusu Msalaba, wacha mwenyewe apitie mchakato huo. Yesu alipokuwa akichapwa na kupigwa, Petro alikuwa akitambuliwa kama mmoja wa wafuasi wake lakini alikana.

> Alipotoka nje kufika kwenye lango, mtumishi mwingine wa kike alimwona, akawaambia watu waliokuwapo, "Huyu mtu alikuwa pamoja na Yesu Mnazareti.'' (72) Akakana tena kwa kiapo akisema, **"Mimi simjui huyo!**'' Mathayo 26:71-72

Kukubali uhakika wa uchungu na mateso ya Kristo kunahusisha kujisalimisha kikamilifu kwa nafsi kutembea naye na kuja kwa ushirika wa mateso yake kwa kuwajali wengine. Mtume Paulo alishika ukweli huu aliposema:

> Zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara tupu nikiyangalinisha na faida kubwa ipitayo kiasi ya kumjua Kristo Yesu Bwana wangu, ambaye kwa ajili Yake nimepata hasara ya mambo yote, nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nimpate Kristo, (9) nami nionekane mbele Zake nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu kwa njia ya imani. (10) Nataka nimjue Kristo na uweza wa kufufuka Kwake **na ushirika wa mateso Yake, ili nifanane naye katika mauti Yake.** Wafilipi 3:8-10

Ili kuwa na maisha yaliyohuru kutoka kwa mateso haya lazima ujifanye kwamba hayapo kisha lazima ujaribu na uyatupilie mbali. Kama unataka kuwa na "maisha ya burudani" yaliyo na msisimko mwingi, radhi na karamu basi lazima usahau kuhusu Msalaba. Kama unataka kumiliki mali nyingi na kuwa tajiri, lazima utende kwa namna ya kusahau Msalaba kwa sababu Msalaba huweka vitu hivi vyote kwa mtazamo wa sio kitu na ni ubatili.

Yesu alijaribu kuwaandaa wanafunzi wake waovo kwa uzoefu wao wa kiwewe kupitia kwa mfano wa wanawali kumi.

> "Wakati huo, Ufalme wa Mbinguni utakuwa kama wanawali kumi waliochukua taa zao na kwenda kumlaki bwana arusi. (2) Watano wao walikuwa wapumbavu na watano walikuwa wenye busara. (3) Wale wapumbavu walichukua taa zao lakini hawakuchukua mafuta ya akiba, (4) lakini wale

> wenye busara walichukua taa zao na mafuta ya akiba kwenye vyombo. (5) Bwana arusi alipokawia kuja wale wanawali wote wakasinzia na kulala. Mathayo 25:1-5

Muda mfupi baada ya hili Yesu alisherehekea Pasaka Alahamisi jioni na kisha akaenda Gethsemane kusali. Hali iliyomzingira Kristo ilikuwa nzito. Wanafunzi wangeona kwamba amelemewa sana. Alimchukua Petro, Yakobo na Yohana pamoja naye katika pahali palipojifisha zaidi kusali.

> Akamchukua Petro pamoja na wale wana wawili wa Zebedayo, naye akaanza kuhuzunika na kufadhaika. (38) Kisha Yesu akawaambia, "Moyo wangu umejawa na huzuni kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mkeshe pamoja nami.'' (39) Akaenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi akaomba, akisema, "Baba yangu, kama inawezekana, kikombe hiki na kiniepuke, lakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo Wewe.'' Mathayo 26:37-39

Ingawa wanafunzi waliona kwamba Yesu alikuwa katika dhiki nyingi walisinzia na wakalala! Baada ya kusali kwa uchungu mwingi kwa kipindi na kutafuta faraja ya ubinadamu Yesu alirudi kwa wanafunzi wake waliokuwa wakilala na anawagutusha kwa maneno:

> **Kisha akarudi kwa wanafunzi wake na kuwakuta wamelala. Akamwuliza Petro, "Je, ninyi wanaume, hamkuweza kukesha pamoja nami kwa saa moja?** (41) ''Kesheni na mwombe, msije mkaanguka majaribuni. Hakika roho iko radhi lakini mwili ni dhaifu.'' Mathayo 26:40-41 (KJV)

Ujasiri wa Petro awali ulikuwa umeonyesha kwamba alikuwa tayari kufa kwa ajili ya Yesu lakini wakati Yesu alipokuwa akifa kwa uzani wa dhiki, alilala. Mbona afanye hivi?

Ili asili ya mwanadamu kudumisha matarajio yake yakiwa hai lazima yalale kwa mateso ya Kristo. Kama tukiwa macho kwa Mateso ya Kristo na tuhisi kwa ajili yake basi tutakesha naye na tutasalimisha matarajio yetu na hamu ya vitu vya ulimwengu huu.

Kila siku tunakaribishwa kufikiria dhabihu ya Yesu kutuvuta kutoka kwa hali ya ubinafsi wetu. Katika huduma ya Agano la Kale kulikuwa na dhabihu ya asubuhi na jioni. Ya asubuhi ilitolewa kitu saa tatu asubuhi na dhabihu ya jioni ilitolewa saa tisa jioni. Saa hizi zilimudu kwetu fursa ya kuwaza kuhusu Mateso ya Kristo na kuomba neema na ujasiri wa kukoma kumsababishia uchungu kwa kuzungumza na kutenda mambo yanayomchoma.

Tutazungumza zaidi kuhusu dhabihu katika muda usiomrefu lakini tunaona kwamba wafuasi wa Kristo waliendelea kukusanyika pamoja kusali katika wakati maalum wa siku tukianza kutambua maana ya Danieli kwamba dhabihu na matoleo ilikuwa imekoma.

> Siku moja Petro na Yohana walikuwa wanapanda kwenda hekaluni kusali yapata saa tisa alasiri. Matendo 3:1

Saa ya maombi ilikuwa wakati wa dhabihu ya jioni lakini mitume walienda kusali tu na kutafakari kuhusu mateso ya Kristo na kuomba neema ili kumuishia.

Kama wewe ni mfuasi wa Yesu Kristo nakukaribisha ukome mara mbili na kutenga wakati kiasi kuwaza mateso makubwa ambayo Baba yetu na mkombozi wanapitia katika uchungu wa wana wao katika ulimwengu wote. Yesu anauliza hivi leo “unaweza kukesha pamoja nami kwa saa moja?”

## 5. Dhabihu na Matoleo Hukupendezwa Nazo

Moja wapo ya sababu kuu ambayo moyo wa kuvunjika kwa kweli kwa msalaba unakosekana ni kwa sababu ya taasisi ya mfumo wa kutoa kafara katika Agano la Kale.

> Semeni na mkutano wote wa Israeli, mkawaambie, Siku ya kumi ya mwezi huu **kila mtu atatwaa mwanakondoo,** kwa hesabu ya nyumba ya baba zao, mwana-kondoo kwa watu wa nyumba moja; (4) na ikiwa watu wa nyumba ni wachache kwa mwana-kondoo, basi yeye na jirani yake aliye karibu na nyumba yake na watwae mwana-kondoo mmoja, kwa kadiri ya hesabu ya watu; kwa kadiri ya ulaji wa kila mtu, ndivyo mtakavyofanya hesabu yenu kwa yule mwana-kondoo. (5) Mwana-kondoo wenu atakuwa hana ila, mume wa mwaka mmoja; mtamtwaa katika kondoo au katika mbuzi. (6) Nanyi mtamweka hata siku ya kumi na nne ya mwezi ule ule; na kusanyiko lote la **mkutano wa Israeli watamchinja jioni.** (7) Nao watatwaa baadhi ya damu yake na kuitia katika miimo miwili na katika kizingiti cha juu, katika zile nyumba watakazomla. Kutoka 12:3-7

> Utanifanyia madhabahu ya udongo, nawe utatoa dhabihu zako juu yake; **sadaka za kuteketezwa, na sadaka za amani**, kondoo zako, na ng'ombe zako, kila mahali nitakapotia ukumbusho wa jina langu, hapo ndipo nitakapokujilia **na kukubarikia**. Kutoka 20:24

Wazo ambalo mafungu haya yanatoa ni kuwa Mungu anataka watu kuwaua Wanyama kama dhabihu kwake na kwamba watakapofanya hili atawabariki. Yohana mbatizaji alimwasilisha Masihi kwa ulimwengu kama mwanakondoo wa Mungu.

> Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu akimjia akasema, "**Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu** aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Yohana 1:29

Kama Yesu ni mwana kondoo wa Mungu aliyetolewa dhabihu basi madai ya mantiki ambayo watu wengi hujenga ni kwamba Mungu alitaka Mwanawe auawe ili kulipia dhambi zetu. Katika dhana hii mwanadamu hamuui Mwana wa Mungu bali kutenda atakalo.

> **Lakini Bwana aliridhika kumchubua; Amemhuzunisha; Utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi,** Ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, Na mapenzi ya Bwana yatafanikiwa mkononi mwake. Isaya 53:10

Kama ilimpendeza Bwana kumponda Mwanawe Msalabani katika dhabihu basi wazo ambalo wengi hupokea ni kwamba Mungu alihitaji dhabihu ili kuridhisha hasira yake dhidi ya dhambi zetu. Hoja ni kuwa haki ya Mungu ilihitaji kuridhishwa. Ili kuonyesha jinsi dhambi zetu zilivyo mbaya, Yesu lazima angechukua nafasi yetu katika kifo ili kuridhisha haki ya Baba. Wimbo maarufu sana wa kikristo huonyesha wazo hili ifuatavyo:

In Christ alone, who took on flesh
Fullness of God in helpless babe
This gift of love and righteousness
Scorned by the ones He came to save
**'Til on that cross as Jesus died**
**The wrath of God was satisfied**
For every sin on Him was laid
Here in the death of Christ I live, I live[4]

Wazo hili la Msalaba hufurukuta mambo kikamilifu. Humwasilisha Mungu kama ambaye huhitaji kifo na hili hutufichia ukweli kuhusu maumbile yetu kama tulivyojadili katika sura ya pili. Kama Mungu alihitaji kifo cha Mwanawe kwa ajili ya dhambi zetu basi chuki yetu asili kwake imechujukwa. Mwanzo tunaweza waza kuwa ni hao Wayahudi na Warumi waliomuua. Pili inaweza semekana kwamba walikuwa wakitekeleza tu kile ambacho Mungu alitamani ili dhabihu ikamilishwe. Ni kwa msatari huu wa mawazo ndio tunapata dhana kama ifuatayo.

---

[4] In Christ Alone. By Natalie Grant 2008.

> Kulinga na wataalam ambao wamerejeshwa, walitafsiri na kuthibitisha muswada, uitwao injili iliyopotea ya Yuda unasema kwamba **Yesu alimwagiza rafiki yake wa karibu Yuda Iscarioti kumsaliti kwa warumi kwa sababu alitaka kutoweka kutuka kwa jela ya mwili wake wa duniani.** Kurasa 26 pages – karatasi 13 za papyrus zilizo na maandishi pande za mbele na nyuma – zinamuonyesha Yuda kama shujaa wa Ukristo, sio kama mbaya.
>
> Uwepo wa hati hii ulidhihirishwa jana kule Washington katika mkutano wa habari uliofanywa na National Geographic Society, ambao ulikuwa sehemu ya jitihada za kitaifa kuokoa nakala pekee ambayo inajulikana kuweko. Ilikuwa imeharibiwa vibaya sana katika safari ya kuajabisha kutoka kwa sanduku la mawe ya chokaa katika kaburi la Mmisri kwa amana salama katika Hicksville, N.Y.
>
> "**Injili ya Yuda hugeuza tendo la Yuda la uasi kuwa tendo la utiifu**," alisema Craig Evans, profesa wa mafunzo ya Agano la Kale katika Chuo cha Acadia Divinity katika Wolfville, N.S., ambaye alisaidia kufasiri hati hiyo.[5]

Kwetu sisi wale ambao tunaamini Bibilia ni Neno la Mungu, wazo kama hilo liko mbali sana na ukweli. Ila swali linasalia, Mungu alihitaji dhabihu hizi? Haki yake inahitaji hili?

> **Dhabihu na matoleo hukupendezwa nazo**, Masikio yangu umeyazibua, Kafara na sadaka za dhambi hukuzitaka. Zaburi 40:6

Bibilia inaelezea wazi kwamba Mungu hakuhitaji dhabihu, pia inaonyesha kwamba hakuhitaji sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya dhambi. Zaidi ya hili tunasoma:

[5] Anne McIlroy, Was Judas a true Christian hero? The Globe and Mail April 7, 2006

> **Maana sikusema na baba zenu, wala sikuwaamuru kwa habari za sadaka za kuteketezwa na dhabihu, siku ile nilipowatoa katika nchi ya Misri; (**23) lakini naliwaamuru neno hili, nikisema, Sikilizeni sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu nanyi mtakuwa watu wangu; mkaende katika njia ile yote nitakayowaamuru mpate kufanikiwa. Yeremia 7:22-23

Mungu anawezaje sema kwamba hakuwaamuru wana wa Israeli kuhusu sadaka za kuteketezwa na dhabihu wakati inaoneka bila shaka aliwaamuru kutoa Pasaka na kuanzisha mfumo wa kutoa kafara? Je, Bibilia injipinga yenyewe hapa?

> Kesho, wakati kama huu, nitakuletea mtu kutoka nchi ya Benyamini, nawe mtie mafuta ili awe mkuu juu ya watu wangu Israeli, naye atawaokoa watu wangu na mikono ya Wafilisti; maana nimewaangalia watu wangu, kwa sababu kilio chao kimenifikilia. (17) **Hata Samweli alipomwona Sauli, Bwana akamwambia, Huyu ndiye niliyekuambia habari zake; huyu ndiye atakayewamiliki watu wangu**. 1 Samweli 9:16-17

Katika kisa hiki Mungu anamwamuru nabii wake Samweli kumteua mtu kuwa mfalme juu ya watu wa Israeli. Katika muktadha matumizi inaonekana kwamba Mungu ndiye anayeamuru mambo hayo. Muktadha mpana ni kwamba Waisraeli walitaka mfalme na Mungu akawatimizia *hitaji lao*.

> **Lakini neno hilo likawa baya machoni pa Samweli, waliposema, Tupe mfalme atuamue.** Naye Samweli akamwomba Bwana. (7) **Bwana akamwambia Samweli, Isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokuambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao**. (8) Kwa kadiri ya matendo yote waliyonitenda tokea siku ile nilipowatoa katika Misri hata leo, kwa kuniacha mimi, na kwa kutumikia miungu mingine, ndivyo wanavyokutenda wewe. 1 Samweli 8:6-8

Bibilia inathibitisha kwamba Mungu hakutaka kuwapa Waisraeli mfalme bali aliwaruhusu kuwa naye.

> Haya ndiyo maangamizo yako, Ee Israeli, ya kuwa wewe u kinyume changu mimi, kinyume cha msaada wako. (10) Yuko wapi sasa mfalme wako, apate kukuokoa katika miji yako yote? Na hao waamuzi wako, uliowanena hivi, Nipe mfalme na wakuu? (11) **Nimekupa mfalme katika hasira yangu**, nikamwondoa katika ghadhabu yangu. Hosea 13:9-11

Ina maana gani kwamba Mungu aliwapa Waisraeli katika hasira yake? Hasira ya Mungu ni kuruhusu mtu apate mambo yasiyosawa ambayo mtu anatamani.[6] Hivyo Bibilia inaonyesha katika sehemu kadhaa Mungu akiamuru vitu kwa mtu ambavyo mtu anatamani. Angazia mfano mwingine.

> Kisha Bwana akanena na Musa, akamwambia, (2) Tuma watu, ili waende wakaipeleleze nchi ya Kanaani, niwapayo wana wa Israeli; katika kabila ya baba zao mtamtuma mtu mmoja, kila mtu na awe mkuu kati yao. Hesabu 13:1-2

Tukisoma kisa hiki katika muktadha wa matumizi yake inaonekana kwamba Mungu alitaka Waisraeli wakaipeleleze nchi ya Kanani. Lakini tunaposoma katika muktadha mpana tunaona jambo tofauti.

> **Nanyi mkanikaribia kila mmoja wenu, mkasema, Na tupeleke watu mbele yetu, ili watupelelezee nchi** na kutuletea habari za njia itupasayo kuipandia, na za miji tutakayoifikia. Kumbukumbu 1:22

Ni Waisraeli ndio ambao walitaka kupeleleza nchi hivyo Mungu aliwaamuru kufanya kile walichotaka. Mbona Mungu afanye hili?

> Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi. Rom 5:20

---

[6] Kwa somo pana juu ya hili tazma sura ya 13 ya kitabu *Matendo ya Mungu wetu mpole* kinachopatikana kwa fatheroflove.info

Mtu anapokuwa na dhambi moyoni mwake kazi ya kwanza ya Mungu nikumuonyesha mtu huyo dhambi yake. Moyo wa mwanadamu uko na uwezo wa kujidanganya. Umepofushwa kuona dhambi zake. Tunapokuwa nje ya matakwa ya Mungu, ataamrisha vitu ambavyo tunavyotaka ili tukue na kuanza kuona mbona tuwaovu. Lakini hafanyi jambo hili bila fursa ya mtu kujua kwamba mambo haya sio sahihi. Amri zinatafsiriwa na watu kumaanisha Mungu hupendezwa navyo kwa sababu watu wamepofushwa kwa dhambi zao wenyewe. Pia wanachagua kuamini hili kwa sababu wakati huo humfanya Mungu kuonekana kama wao na hili hutia haki uovu wao.

Tunagundua katika sura ya pili kwamba mbegu za mauti zilikuwa moyoni mwa Adamu. Alimshtaki Mwana wa Mungu kwa wajibu wa matendo ambayo aliamini kwamba yalidai hukumu ya kifo na akahofu kuwa Mungu angeiweka juu yake. Ili kuepuka kifo alielekeza lawama juu ya mke wake. Alikuwa radhi kwake kufa kwa niaba yake. Adamu alidhani kwamba haki ya Mungu ilihitaji kifo. Pia aliwaza kwamba lawama ingegeuzwa na kwamba mwingine angelipa deni ambayo aliamini Mungu alidai. Ili Adamu aone kilichokuwa moyoni mwake, Mungu aliagiza mfumo wa kutoa dhabihu. Mfumo wa kutoa dhabihu ni akisi wa kile ambacho mtu anafikiria. Mfumo wa kutoa dhabihu ni kioo kwa akili za mtu. Katika muktadha huu unaweza leta uiano wa mafungu ya Bibilia kuhusu dhabihu.

> Naye Samweli akasema, je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu Sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia kuliko mafuta ya beberu. 1 Samwiel 15:22

Mungu anataka tu tumwamini na kumtii kwa kuamini katika neema yake. Hakupenda kuwapa watu dhabihu lakini aliagiza kwamba kilichokuwa katika moyo wa mtu kumuonyesha dhambi zake. Lakini mbona Mungu akampa Musa maagizo haya marefu kuhusu mfumo wa kutoa dhabihu?

> Nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu. Hayo ndiyo maneno utakayowaambia wana wa Israeli. (7) Musa akaenda akawaita wazee wa watu, akawafunulia maneno

> hayo yote, Bwana aliyokuwa amemwagiza. (8) **Watu wote wakaitika pamoja wakisema, Hayo yote aliyoyasema Bwana tutayatenda.** Naye Musa akamwabmbia Bwana maneno ya hao watu. Kutoka 19:6-8

Bwana alipowajia Waisrael alitaka wote wawe makuhani nakuamini katika neema yake na kuwapa ahadi zote za agano. Lakini Waisraeli walimwambia Mungu kwamba kila kitu ambacho aliahidi kuwapa walimwahidi kutenda badala yake. Kwa muda wa majuma walikuwa wamevunja ahadi zao kwa kucheza ngoma wakimzunguka ndama wa dhahabu. Kwa hasira Musa alivunja mbao za amri kumi ambazo Mungu alikuwa amekata bila mikono na kuandika juu yake.

> Kisha Bwana akamwambia Musa, **Chonga mbao mbili za mawe mfano wa zile za kwanza; nami nitaandika juu ya mbao hizo** maneno hayo yaliyokuwa juu ya mbao za kwanza, hizo ulizozivunja. Kutoka 34:1

Jozi la pili la amri lilikuwa limetengenezwa kwa mikono ya mwanadamu na Mungu akaandika juu yake. Inawakilisha muungano wa kazi ya Mungu na kazi ya Mwanadamu. Watu walikuwa wamekataa neema ya Mungu ya kujitolea kila kitu bure. Walitaka kujifanyia ili kuonyesha ucha Mungu wao na wema. Kwa hivyo Mungu aliwaamuru vitu ambavyo vilikuwa mioyoni mwao ili kufanya dhambi kuwa nyingi. Mioyo yao ilikuwa imejawa na dhabihu na sadaka. Sio hili ambalo walifanya wakimzunguka ndama wa dhabu? Hivyo Mungu aliwapa amri kuwaonyesha kiwango cha akili yao ya kidunia.

> Tena naliwapa amri zisizokuwa njema, na hukumu ambazo hawakuweza kuishi kwazo; Ezekieli 20:25

Inakuwaje kwamba Mungu anapeana vitu kwa watu wake ambavyo hawawezi kuishi navyo? Huwapa vitu ambavyo wanataka. Ni u mbali upi akili ya mwanadamu inaweza safiri ili kujaribu na kumtuliza Mungu kwa dhabihu?

> Ndipo mfalme na watu wote wakatoa dhabihu mbele za Bwana. (5) **Mfalme Sulemani akatoa sadaka ya ng'ombe ishirini na mbili elfu, na kondoo mia na ishirini elfu.** Ndivyo mfalme na watu wote walivyoifanya wakfu nyumba ya Mungu. 2 Nyakati 7:4-5

Ni wapi Mungu alihitaji vitu hivi? Bibilia inasema Mungu hakutaka dhabihu na sadaka. Hapo mwanzo alimwamuru Adamu mara moja kwa mwaka angalau atoe mwana kondoo kumuonyesha kilichokuwa moyoni mwake.

> Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana. (4) Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake, Mwanzo 4:3-4

Tafsiri ya hapo juu inasema kwamba ilipokuwa wakati wa mavuno wangekuja na kutoa sadaka zao.

> **Ikawa hatimaye** Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana; Mwanzo 4:3

Kusoma halisi ni kwamba katika mwisho wa siku au mwisho wa mwaka na huu ndio wakati ambao uvunaji ulitendeka. Mnyama mmoja kwa mwaka kwa kila familia anageukaji kuwa wana kondoo 120,000 na ng'ombe 22,000 wanaotolewa na mfalme? Wanadamu walikuwa tayari kuwatoa wana wao kafara ili kumfurahisha mungu ambaye walimfikiria. Andiko linasemaje?

> **Je! Bwana atapendezwa na elfu za kondoo waume, au na elfu kumi za mito ya mafuta? Je! Nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, mzao wa mwili wangu kwa dhambi ya roho yangu?** (8) Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako! Mika 6:7-8

Mungu alitaka watu wamwamini na waipokee neema yake ya kutii. Hakuhitaji dhabihu kumtuliza. Kifungu kinachokuja mawazoni kama itikio kwa hili ni kifuatacho:

> Kwa kweli sheria hudai kwamba, karibu kila kitu kitakaswe kwa damu, wala pasipo kumwaga damu, hakuna msamaha wa dhambi. Waebrania 9:22

Mbona sheria inafundisha kwamba bila umwagikaji wa damu hakuna ondoleo la dhambi, msamaha, au uhuru? Kwa sababu sheria ni kioo cha kuonyesha kilicho moyoni mwa mwanadamu.

> Kwa hiyo hakuna binadamu hata mmoja atakayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa matendo ya sheria, **kwa maana sheria hutufanya tuitambue dhambi**. Warumi 3:20

Sio kwa matendo ya kutoa dhabihu ya sheria ndio watu wanahesabiwa haki mbali ni kupitia kwa kuona kwamba kutoa dhabihu ndiyo hali yetu na kisha tutubu dhambi hii. Sheria huweka mbegu wazi ili iweze kuungamwa. Sio Mungu ambaye huhitaji "bila umwagikaji wa damu" hakuwezi kuwa na msamaha ila ni mwanadamu ndiye huamini hili na hawawezi amini kwamba Mungu atamsamehe isipokuwa ametoa dhabihu. Kwa wale ambao wanamasikio ya kusikia wacha waelewe.

Hivyo sheria kuhusiana na dhabihu inatupa ufahamu wa moyo wa dhambi wa mwanadamu. Tunakumbuka kile Andiko linasema:

> Maana sikusema na baba zenu, wala sikuwaamuru kwa habari za sadaka za kuteketezwa na dhabihu, siku ile nilipowatoa katika nchi ya Misri; Yeremia 7:22

Njia pekee ya kuleta uiano katika kauli hii na kila kitu ambacho kimeandikwa katika Torah ni kufahamu kwamba Torah ni kioo cha utulizo kwa msingi wa akili ya mwanadamu na kumuonyesha dhambi hii ndani yake.

Licha ya hali mbaya ya mwanadamu ikitaka kutoa dhabihu na kuua kitu kumtuliza Mungu, kupitia kwa uharibifu huu Mungu aliweza kumfundisha mwanadamu kuhusu kuwa radhi kwake kumsamehe na kuwaelekeza kwa Masihi ajaye ambaye ataonyesha tabia za mwana kondoo. Ufunuo wa tabia hii utageuza mioyo ya watu kwa Mungu. Kwa maana tabia ya Mungu ilidhihirishwa katika Kristo ambayo hugeuza mioyo ya watu kumwelekea Mungu na kuwafanya kuwa wamoja. Hii ndio maana Yesu alisema usiku ule kabla afe:

> Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. (4) Nimekutukuza Wewe duniani **kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye**. Yohana 17:3-4

Kama Kristo alitimiza kazi ambayo Baba yake alimpa kuifanya usiku kabla ya kufa basi Mungu hakutaka Mwanawe afe, alihitaji tu kutuonyesha tabia yake ya upendo na rehema. Watu walihitaji Kristo afe kwa sababu kwetu, katika hali yetu halisi hakuwezi kuwa na msamaha bila adhabu. Ili tukubali msamaha wa Mungu jamii ya mwanadamu lazima ingemuona Yesu akifa. Hivyo kabla Yesu kufa alilia.

> Baada ya kuionja hiyo siki, Yesu akasema, **"Imekwisha."** Akainamisha kichwa chake, akakata roho Yohana 19:30

Nini kilikwisha? Alikuwa ametenda kile ambacho wanadamu walihitaji kuona ili waamini wanaweza samehewa. Hii ndio sababu mbona Mungu aliamuru dhabihu, kwa maana watu walihitaji kuona na kuamini kwamba mtu angekufa kama mbadala wao.

Kufahamu ukweli muhimu wa swali hili ni kuwasilisha Msalaba wa Kristo katika nuru ya tofauti ya zote kwa pamoja; nuru iliyo safi, ya thamani na ya kuweka huru. Je, utaingia katika nuru hii?

# 6. Sisi Tunayo Sheria

Katika kabiliano moja na viongozi wa Israeli, Yesu alisema:

> **Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba yenu**. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hakushikana na kweli maana hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo *yake mwenyewe* kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo uongo. Yohana 8:44

Viongozi wa Israeli walipozungumza na Yesu, walizungumza maneno ya Shetani kwa sababu Yesu aliwaambia kuwa Shetani alikuwa baba yao na kwa hivyo wangetenda matakwa ya baba yao Shetani. Maneno haya ya viongozi wa Wayahudi yanaonyesha mawazo ya Shetani na uelewa wote wa mwanadamu wa haki.

> Wayahudi wakamjibu, ''**Sisi tunayo sheria na kutokana na sheria hiyo, hana budi kufa** kwa sababu Yeye alijiita Mwana wa Mungu.'' Yohana 19:7

> Mmoja wao, aliyeitwa Kayafa, ambaye alikuwa Kuhani Mkuu mwaka huo akasema, "Ninyi hamjui kitu cho chote! (50) Hamjui kwamba ni afadhali **mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, kuliko taifa lote liangamie?''** Yohana 11:49-50

Viongozi wa Israeli walikuwa wamemhukumu Yesu mawazoni mwao. Kulingana na kusoma kwao kwa sheria, Yesu alistahili kifo. Nikodemu alikata rufaa kwa viongozi wenzake kwa swali hili.

> **Je, sheria zetu zinaturuhusu kumhukumu mtu** kabla ya kumsikiliza na kufahamu alilotenda? Yohana 7:51

Wangemuua Yesu mapema zaidi isipokuwa ni kwa utawala wa Roma katika nchi yao.

> Pilato akawaambia, "Basi mchukueni ninyi mkamhukumu kwa kufuata sheria zenu.'' Wayahudi wakamjibu, ''Sisi

> haturuhusiwi kutoa hukumu ya kifo kwa mtu ye yote.’ Yohana 18:31

Jinsi viongozi walivyo itafsiri sheria ya Musa ilikuwa kuweka adhabu ya kifo kwa wale walioasi sheria. Sheria nyingi ziliweka adhabu ya kupigwa mawe. Yesu alipoitafsiri sheria ya Musa aliitumia sheria kwa njia tofauti.

> Walimu wa sheria na Mafarisayo wakamleta mwanamke mmoja aliyefumaniwa akizini. Wakamsimamisha katikati ya umati wa watu wote. (4) Wakamwambia Yesu, “Mwalimu, huyu mwanamke amekutwa akizini. (5) **Katika sheria, Mose alituamuru kuwapiga kwa mawe wanawake wa namna hii, mpaka wafe.** Sasa Wewe wasemaje?’’ (6) Walimwuliza swali hili kama mtego ili wapate sababu ya kumshtaki. Lakini Yesu akainama akaanza kuandika ardhini kwa kidole Chake. (7) Walipoendelea kumwulizauliza akainuka, akawaambia, “**Kama kuna mtu ye yote miongoni mwenu ambaye hana dhambi na awe wa kwanza kumtupia jiwe.’’** (8) Akainama tena na kuandika ardhini. (9) Waliposikia haya, wakaanza kuondoka mmoja mmoja, wakianzia wazee, hadi Yesu akabaki peke Yake na yule mwanamke akiwa amesimama mbele Yake. (10) Yesu akainuka na kumwambia, **“Wako wapi wale waliokuwa wanakuhukumu kuwa mwenye hatia?**’’ (11) Yule mwanamke akajibu, “Hakuna hata mmoja Bwana.’’ Yesu akamwambia, **“Hata Mimi sikuhukumu**. Nenda zako, kuanzia sasa usitende dhambi tena. Yohana 8:3-11

Mafarisayo walimshika mwanamke huyu (na mwanamume katika hali hiyo) katika kitendo hicho. Kulingana na uelewa wao wa sheria alipaswa kupigwa mawe hadi kufa. Yesu aliandika ardhini kama njia ya kuwatia hatiani. Katika kuwaambia kuwa walihitaji kuishi bila dhambi ili kuwa na haki ya kinidhamu kumpiga mawe, walitiwa hatiani na dhambi zao wenyewe. Badala ya kuomba msamaha walijikemea wenyewe na kuondoka mbele yake. Alimsamehe mwanamke bure na kumkaribisha asitende dhambi tena. Hili lilimletea mwanamke huyu pumziko na shukurani kwa Mkombozi wake. Kristo alitumia sheria kuokoa ilhali Mafarisayo waliitumia kuua.

Hili linadhihirisha tofauti kati ya haki ya Mungu na Haki ya Shetani. Watu wengi huamini kuwa haki ya Mungu huhitaji kifo. Wanaamini kuwa rehema na haki ziko katika upinzani wa kila moja na kuwa wakati ambao rehema ya Mungu inapoonekana ikitenda kwa mkono wake mrefu wa sheria yake huvunja wale wenye hatia.

Wacha tuangazie Maandiko.

> [1] Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako: [2] Fadhili na kweli zahudhuria mbele za uso wako. Zaburi 89:14

Zingatia koloni baada ya neno kiti chako. Koloni hutenganisha vishazi huru viwili ambapo kishazi cha pili kinaelezea cha kwanza. Hili linaelezea kuwa haki ya Mungu ni kuonyesha rehema. Haki ni kutenda jambo la haki na jambo la haki kwa Mungu kutenda ni kuonyesha rehema kwa nuru ya ukweli. Swali ni, haki ya Mungu inadumu kwa muda gani?

> Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; **Rehema zake ni za milele**; Na uaminifu wake vizazi na vizazi. Zaburi 100:5

> Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema; **Kwa maana fadhili zake ni za milele.** (2) Mshukuruni Mungu wa miungu; Kwa maana fadhili zake ni za milele. (3) Mshukuruni Bwana wa mabwana; **Kwa maana fadhili zake ni za milele**. (4) Yeye peke yake afanya maajabu makuu; **Kwa maana fadhili zake ni za milele**. (5) Yeye aliyefanya mbingu kwa fahamu zake; Kwa maana fadhili zake ni za milele; Zaburi 136:1-5

Kutoka kwa mtazamo wa Mungu, rehema yake haiishi kamwe, lakini kwa wale ambao wanamkataa hakuna mungu mwingine mwenye rehema, hivyo wanatarajia kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao na Mungu huruhusu uchaguzi wao mbaya kuwapiku, hivyo basi kuruhusu maana yao ya haki kutimizwa.

> Bwana amejidhihirisha na kutekeleza hukumu; Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake. Zaburi 9:16

Ni nini hukumu ya Mungu kwa waovu? Huwaruhusu kuangukia matokeo ya uamuzi wao. Hazui hili. Hilo ndilo jambo nzuri kutenda, sivyo? Kama wanaweza omba rehema anaweza wapitishia rehema ili kuwasaidia kuvuka matokeo lakini kama hawatarajii rehema yoyote na hawaombi rehema basi hawawezi ipokea hata ikitolewa. La kuhuzunisha watu wengi hufikiria kuwa Mungu ni kama sisi. Wanafikiria kuwa Haki ya Mungu ni sawa na haki yetu.

> Ndivyo ulivyofanya, nami nikanyamaza; Ukadhani ya kuwa Mimi ni kama wewe. Walakini nitakukemea; Nitayapanga hayo mbele ya macho yako. Zaburi 50:21

Kama haki ya Mungu ilihitaji kifo basi Mungu angekuwa muumbaji wa kifo. Kama Mungu angekuwa na kusudi la kuchukua uhai wa mmoja wa viumbe alivyoumba kwa kuvunja sheria basi kanuni ya kifo inadumu ndani ya Mungu. Lakini tunapomtazama Yesu ufunuo wa Baba tunaona uzima tu. Hatuoni kifo.

> Yesu akamwambia, "**Mimi ndiye huo ufufuo na uzima.** Yeye aniaminiye Mimi, hata akifa atakuwa anaishi Yohana 11:25

> Tunawajulisha lile lilokuwako tangu mwanzo, lile tulilosikia,ambalo tumeliona kwa macho yetu, ambalo tumelitazama na kuligusa kwa mikono yetu, kuhusu Neno la Uzima, (2) **Uzima huo ulidhihirishwa, nasi tumeuona na kuushuhudia, nasi twawatangazieni uzima wa milele, ambao ulikuwa pamoja na Baba, nao ukadhihirishwa kwetu**— 1 Yohana 1:1-2

Mungu hakuumba agizo la kifo kwa dhambi. Dhambi ni ya kuangamiza yenyewe. Mshahara wa dhambi ni mauti. Ni jambo ambalo linatamaniwa kwa kuhusika katika dhambi. Mungu halipi mshahara wa dhambi, dhambi hulipa. Bibilia haisemi kwamba mshahara KWA dhambi ni mauti, inasema mshahara WA dhambi ni mauti. Tofauti ni kubwa.

Bibilia inatudhihirishia kupitia visa vya Agano la Kale jinsi agizo la kifo liliingia ulimwenguni.

> Kwa maana kila kitu kilichoandikwa zamani, kiliandikwa kutufundisha, ili kwamba kwa saburi na faraja tunayopata katika Maandiko tuwe na tumaini. Warumi 15:4

Shetani ndiye mzalishi wa amri ya kifo kwa waasi. Tunagundua katika kisa cha Danieli na tundu la Simba mchakato wa jinsi amri ya kifo ilianzishwa.

> Ilimpendeza Dario kuweka juu ya ufalme maliwali mia na ishirini, wawe juu ya ufalme wote; (2) na juu yao akaweka wakubwa watatu, na Danielii alikuwa mmoja wao; ili maliwali hawa watoe hesabu kwao, mfalme asipate hasara. (3) **Basi Danielii huyo alipata sifa kuliko wakubwa na maliwali**, kwa kuwa roho bora ilikuwa ndani yake; **naye mfalme akaazimu kumweka juu ya ufalme wote.** (4) Basi mawaziri na maamiri wakatafuta sana kupata sababu za kumshitaki Danielii kwa habari za mambo ya ufalme; lakini hawakuweza kuona sababu wala kosa; kwa maana alikuwa mwaminifu, wala halikuonekana kosa wala hatia ndani yake. (5) Ndipo wale watu wakasema, **Hatutapata sababu ya kumshitaki Danielii huyo, tusipoipata katika mambo ya sheria ya Mungu wake**. (6) Basi wale mawaziri na maamiri wakakusanyika pamoja mbele ya mfalme, wakamwambia hivi, Mfalme Dario, uishi milele. (7) **Mawaziri wote wa ufalme, na manaibu, na maamiri, na madiwani, na maliwali wamefanya shauri pamoja ili kuweka amri ya kifalme; na kupiga marufuku, ya kwamba mtu ye yote atakayeomba dua kwa Mungu awaye yote, au kwa mtu awaye yote, katika muda wa siku thelathini, ila kwako, Ee mfalme atatupwa katika tundu la simba.** Danieli 6:1-7

Kisa hiki kimeandikwa kwa mafundisho yetu. Dario ni mfano wa Mungu Baba na Danieli ni mfano wa Kristo. Danieli alikuwa katika wadhifa wa juu baada ya mfalme na mfalme aliwaza kumweka juu ya utawala wote. Jambo hili lilianzisha wivu kwa wale waliokuwa chini ya Danieli. Kupitia kwa wivu huu viongozi waliokuwa chini ya Danieli walibuni amri ya kifo ambayo ilikuwa imelengwa kwa danieli. Mfalme hakuwa amebuni amri hii lakini

iliwasilishwa kwake na akatia sahihi yake bila kujua maana yake. Mungu alijua maana ya jaribio la Shetani la kumwangamiza Kristo ambaye alikuwa juu yake. Shetani alikuwa na wivu kwa Mwana wa Mungu na kuwaathiri wengi wa malaika kujiunga naye katika kujaribu kumbandua Kristo. Shetani alipoivuta jamii ya mwanadamu katika mtego wake, Mungu aliruhusu mpango wa Shetani kufanikiwa na kupelekea kwa kifo cha Kristo. Sehemu kubwa ya ulimwengu hufikiria kuwa kifo cha Kristo nikuridhisha mahitaji ya mfalme lakini ilikuwa kudhihirisha kusudi la siri la Shetani la kumwangamiza Kristo.

Wakati ambao Shetani alifikiria ungekuwa ushindi mkubwa, alidhihirisha mchoro wake wa mauaji na huruma yake yote mbinguni ilikuwa imeondoka.

> Mfalme akaamuru, nao wakawaleta wale watu waliomshitaki Danielii, wakawatupa katika tundu la simba, wao, na watoto wao, na wake zao; na wale simba wakawashinda wakaivunja mifupa yao vipande vipande, kabla hawajafika chini ya tundu. Danieli 6:24

Dario mfalme aliwapa watu waliopanga mauaji ya Danieli kile kitu hasa walichotamani kumfanyia Danieli. Baba yetu aliyembinguni alimruhusu Shetani kupokea uhalibifu aliyotaka kumpa Kristo. Kristo alikuwa katika tundu la Simba la njia ya Msalaba usiku wote na katika siku iliyofuata. Kama Danieli alitoka katika tundu asubuhi ya ufufuo na kuwashinda waliotafuta kumwangamiza.

Hoja ya kisa hiki ni kuwa ni watu waliokuwa chini ya Mwana wa Mungu walioangua wazo la kifo kwa wale wasiomheshimu Baba. Mungu hakuanzisha mpango huo lakini aliuruhusu ili kudhihirisha mchoro wa Shetani uliokuwa umefichwa kwa kila mmoja. Sheria ya magavana wa Babeli ilikuwa ya kumpa mfalme haki. Ilikuwa iwakilishe haki yake lakini ilikuwa haki ghushi ambayo ilimalizia kuwaangamiza walioiangua.

Katika kisa kingine kutoka Agano la Kale tunaona tofauti kati ya haki ya mfalme na mmoja wa wanawe.

> Tena Absalomu huondoka asubuhi na mapema, na kusimama kando ya njia ya lango; kisha ikawa, mtu ye yote aliyekuwa na neno, lililokuwa halina budi kufika kwa mfalme ili kuhukumiwa, Absalomu humwita mtu huyo kwake, na kumwuliza, Wewe u mtu wa mji gani? Naye akasema, Mtumwa wako ni mtu wa kabila fulani ya Israeli. (3) Naye Absalomu humwambia, Tazama, maneno yako ni mema yenye haki; lakini hapana mtu aliyeagizwa na mfalme kukusikiliza. (4) Tena Absalomu husema, Laiti Mimi ningewekwa kuwa mwamuzi katika nchi hii, ili kila mtu mwenye neno au daawa aje kwangu, nimpatie haki yake! (5) Tena ikawa hapo alipokaribia mtu ye yote kumsujudia, hunyosha mkono wake, na kumshika, na kumbusu. (6) Hivyo ndivyo Absalomu alivyowatendea Israeli wote, waliomwendea mfalme ili wapate hukumu; na hivyo Absalomu akawadanganya watu wa Israeli. 2 Samweli 15:2-6

Jina Absalomu humaanisha *baba wa amani* lakini kilichofichika katika jina hili ilikuwa chuki na vita. Absolomu alitaka babake amwadhibu nduguye wa kambo Amnoni aliye mdulumu dadaye Absalomu, Tamari. Kwa sababu mfalme Daudi hakukata kesi dhidi yake, Absalomu alimdharau babake na akaamua kumbandua. Absalomu alichukua sheria mikononi mwake kumwadhibu kifo Amnoni kwa haki aliyohisi ilikuwa sahihi. Kisha akajipanga kuishinda mioyo ya ufalme wa Israeli.

> Mfalme akamwambia, Kwa nini aende nawe? Lakini Absalomu akamsihi sana, naye akamwacha Amnoni na wana wote wa mfalme waende naye. (28) Kisha Absalomu akawaamuru watumishi wake, akasema, Angalieni basi, moyo wake Amnoni utakapofurahiwa kwa mvinyo; **nami nitakapowaambia, Mpigeni Amnoni, ndipo mwueni, msiogope; si mimi niliyewaamuru? Iweni hodari, iweni na ujasiri.** (29) Basi watumishi wa Absalomu wakamfanyia Amnoni kama alivyoamuru Absalomu. Ndipo wakaondoka wana wote wa mfalme, wakapanda kila mtu nyumbu wake, wakakimbia. 2 Samweli 13:27-29

Shetani ambaye asilia alikuwa Lusifa hakufurahishwa na ukweli kwamba Mwana wa Mungu alitukuzwa. Alihisi kuwa haikuwa haki kwake na akaamua kumwondoa Mwana wa Mungu. Mfalme alipoingilia na kuweka wazi hukumu yake, Lusifa aliamua kung'atua ufalme. Alijishindia malaika wengi kwa upande wake. Suala lililokuwepo wakati huo lilikuwa la haki.

> "Laiti mimi ningewekwa kuwa mwamuzi katika nchi hii, ili kila mtu mwenye neno au daawa aje kwangu, nimpatie haki yake!" 2 Samweli 15:4

Uchongezo wa Absalomu ulikuwa kwamba mfalme hakutoa haki kwa watawaliwa wake lakini madai haya yalikuwa ya uongo. Mwanzoni katika kitabu cha Samweli tunasoma:

> Daudi akatawala juu ya Israeli wote; **naye Daudi akawafanyia hukumu na haki watu wake wote**. 2 Samweli 8:15

Daudi alikuwa akitoa haki kwa watawaliwa wake lakini haikuwa haki ambayo Absalomu alidhania ilihitajika. Daudi alionyesha rehema kwa sababu rehema ya Mungu ilikuwa pamoja naye na kuukuza ufalme wake

> Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele. (14) Mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu; akitenda maovu nitamwadhibu kwa fimbo ya binadamu na kwa mapigo ya wanadamu; (15) **lakini fadhili zangu hazitamwondoka**, kama vile nilivyomwondolea Sauli, niliyemwondoa mbele yako. (16) **Na nyumba yako, na ufalme wako, vitathibitishwa milele mbele yako. Nacho kiti chako kitafanywa imara milele.** 2 Samweli 7:13-16

Absalomu hakutaka ufalme ambao ulijengwa juu ya haki ambayo ilionyesha rehema. Alitaka haki ambayo iliwahukumia kifo bila huruma waliokosea. Kisa hiki kinaakisi vita asilia kule mbinguni. Shetani aliwashawishi malaika wengi kwa mtazamo wake wa haki uliohitajika ili kupata utawala. Absolamu aliwashawishi wenzake kuwa mawazo yake juu ya haki yangeboresha

ufalme na alifanikiwa kuiba mioyo ya watu wa Israeli. Shetani aliiiba mioyo ya malaika wengi na malaika wengine walikuwa na mdadisi kuhusu mawazo yake na kumhurumia. Twajua hili kwa sababu Shetani hakukataliwa kabisa kutoka mbinguni hadi alipomuua Mwana wa Mungu. Ilikuwa ni baada ya hili ndipo akatupwa duniani.

> Luka 10:18 Yesu akawaambia, “Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme wa radi.

> **Mkia wake ukakokota theluthi ya nyota zote angani na kuziangusha katika nchi.** Ndipo lile joka likasimama mbele ya yule mwanamke aliyekuwa karibu kuzaa ili lipate kumla huyo mtoto mara tu atakapozaliwa. (5) Yule mwanamke akazaa mtoto mwanamume, atakayeyatawala mataifa yote kwa fimbo yake ya utawala ya chuma. Lakini huyo mtoto akanyakuliwa na kupelekwa kwa Mungu kwenye kiti Chake cha enzi. Ufunuo 12:4-5

Shetani alikuwa amechukua theluthi moja ya malaika kuwa nao kwa uhalisia. Alivamia kanisa lililokuwa duniani na akajaribu kumla mtoto wake aliyekuwa Mwana wa Mungu katika Bethlehemu. Ni baada ya Yesu kurejea mbinguni ndio Shetani alitupwa kutoka akilini mwa wote kule mbinguni.

> Basi palikuwa na vita mbinguni: Mikaeli na malaika zake wakapigana na hilo joka, nalo joka pamoja na malaika zake likapigana nao. (8) Lakini joka na malaika zake wakashindwa na hapakuwa tena na nafasi kwa ajili yao mbinguni. (9) **Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani, aupotoshaye ulimwenguni wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake.** (10) Kisha nikasikia sauti kuu mbinguni ikisema, “Sasa Wokovu na uweza na Ufalme wa Mungu wetu umekuja na mamlaka ya Kristo wake. Kwa kuwa ametupwa chini mshtaki wa ndugu zetu, anayewashtaki mbele za Mungu usiku na mchana. Ufunuo 12:7-10

Kumekuwa na vita tangia mwanzo wa wakati kati ya Kristo na malaika wake na Shetani na malaika wake. Theluthi moja ya malaika ilimfuata Lusifa katika giza na wakatoka Mbinguni.

> **Nao malaika ambao hawakulinda nafasi zao, lakini wakayaacha makao yaliyokuwa yao hasa**, hawa amewaweka katika giza, wakiwa wamefungwa kwa minyororo ya milele kwa ajili ya hukumu siku ile kuu.. Yuda 1:6

Ni ukweli kuwa Mungu aliwatupa kutoka mbinguni lakini walitupwa kwa uongo walioanza kuuamini (Ufu 12:4). Mungu aliwapa mapenzi ya mioyo yao. Walimfikiria Mungu kuwa mkatili na asiyekuwa na huruma na waliikimbia sura ya uongo waliokuwa nayo wenyewe.

Shetani alikuwa amekusudia kuanzisha enzi yake yeye mwenyewe iliyojumuisha mawazo yake tofauti ya haki. Alitaka kutawala uumbaji wote wa Mungu.

> Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, **Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu**; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. (14) Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu. Isaya 14:13-14

Kisa cha Absalomu kinaashiria kuwa taifa lote liliathiriwa na mawazo yake ya haki.  Ukweli kuwa Shetani angeenda mbinguni kama mwakilishi wa dunia inaashiria kuwa mawazo yake hayakueleweka kikamilifu hata na malaika wa mbinguni.

> Ilikuwa, siku moja ambayo hao wana wa Mungu walikwenda kujihudhurisha mbele za Bwana, Shetani naye akaenda kati yao. (7) Bwana akamwuliza Shetani, Umetoka wapi wewe? Ndipo Shetani akamjibu Bwana, na kusema, Natoka katika kuzungukazunguka duniani, na katika kutembea huku na huku humo. Ayubu 1:6-7

Uwepo wa Shetani katika shauri la kifalme unauhusiano na matendo ya Absalomu katika kuwachukua Masuria wa baba yake na kupitisha mbegu yake kwao kwa jaribio la kutia ila kwa uzao wa kifalme.

> Naye Ahithofeli akamwambia Absalomu, Ingia wewe kwa masuria ya baba yako, hao aliowaacha ili kutunza nyumba; na Israeli wote watasikia ya kuwa umechukizwa kabisa na baba yako; ndipo itatiwa nguvu mikono yao wote walio pamoja nawe. (22) Basi wakamtandikia Absalomu hema juu ya nyumba darini; **naye Absalomu akaingia kwa masuria ya babaye machoni pa Israeli wote.** 2 Samweli 16:21-22

Maneno ya Shetani ni mbegu ya akili na yalikuwa na athari juu ya ulimwengu. Hadi wakati ambao mbegu ya mauaji dhidi ya Mwana wa Mungu iliyodumu ndani ya Adamu iliwekwa wazi miaka 4000 baadaye katika kusulubishwa kwa Kristo, nia ya Shetani haikuwa imejulikana kwa kweli. Hili lilimruhusu Shetani kuhusisha tabia zake mwenyewe na za Mungu. Kadri Shetani angeweza kuficha utambulisho wake alikuwa na uwezo wa kudanganya kuhusu jinsi Mungu alivyo kwa kweli. Ana nguvu hizi kwa sababu alikuwa malaika wa kwanza na malaika wengine walikuwa na imani naye katika ufahamu wa Mungu. Hili ndilo ambalo lilimruhusu kutenda uovu kupitia kwa sheria ya Mungu.

> Je! Kiti cha udhalimu kishirikiane nawe, Kitungacho madhara kwa njia ya sheria? Zaburi 94:20

Shetani aliketi juu ya kiti cha maovu na akatumia sheria ya Mungu kusisitiza kwamba lazima kuwe na amri ya kifo kwa uasi wa sheria. Kisa cha Danieli katika tundu la simba kinadhihirisha mchakato huu. Kisa cha Absalomu kinaonyesha kwamba lilikuwa suala la haki likiendelezwa ili kupata mioyo ya ufalme. Visa hivi vyote ni vya kutafakari kuhusu vita ambavyo vilianzishwa mbinguni na kisha kuingia duniani. Suala katika mgogoro halijabadilika.

Lakini bado baada ya kifo cha Kristo, Shetani aliwekwa wazi kwa nia yake halisi. Kristo alidhihirisha kwa ulimwengu tabia ya upendo wa kweli wa Mungu. Yesu alionyesha kwamba Mungu aliwapenda adui zake; aligeuza

shavu lingine na kwa unyenyekevu alijitiisha kwa kifo cha kutisha zaidi bila kujikinga kwokwote. Matendo ya Shetani na mawakala wake kwa Mwana wa Mungu duniani yaliweka wazi tabia yake. Ufunuo wa Mungu na Kristo kulimuonyesha kuwa kinyume kabisa katika tabia. Hivyo kupitia kifo Kristo aliangamiza ufalme wa yule aliye na nguvu za mauti.

> Basi kwa kuwa watoto wana nyama na damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao, **ili kwa kifo chake, apate kumwangamiza huyo mwenye nguvu za mauti, yaani, Shetani -** Waebrania 2:14

Mafarisayo walikuwa wameathiriwa na mawazo ya Shetani ya haki. Hiyo ndio sababu waliazimia kumua Kristo. Yesu hakutafuta kuwaua wala kutishia kuwaua.

> Kisha Kuhani Mkuu akasimama na kumwambia Yesu, "Je, wewe hutajibu? Ni ushahidi wa namna gani hawa watu wauletao dhidi yako?" (63) Lakini Yesu alikuwa kimya. Ndipo Kuhani Mkuu akamwambia, "Nakuapisha mbele za Mungu aliye hai, tuambie ikiwa wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu." (64) Yesu akajibu, "Wewe umenena. **Lakini ninawaambia nyote, Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenye Nguvu na akija juu ya mawingu ya mbinguni.''** (65) Ndipo Kuhani Mkuu akararua nguo zake na kusema, "Amekufuru! Kwa nini tunahitaji ushahidi zaidi? Tazama, sasa ninyi mmesikia hayo makufuru. (66) **Uamuzi wenu ni nini?" Wakajibu, ''Anastahili kufa"** Mathayo 26:62-66

Yesu anapowaambia Mafarisayo juu ya kuja kwake na utukufu, anatangaza tu kwamba watamuona. Mafarisayo kwa upande mwingine wanamhukumu Kristo kifo. Tofauti ni wazi kabisa. Ushahidi upo kwa wale ambao wanautafuta. Haki ya Mungu haihitaji kifo mbali mfumo wa haki ya Shetani huhutaji. Mungu kumruhusu Mwanawe kufa ni kudhihirisha chuki ya Shetani na mfumo wa haki ya ufalme wake.

Katika muktadha huu msalaba umebadilishwa katika maana yake. Mungu hakuhitaji kifo cha Kristo kuridhisha haki. Ila wanadamu walisema kuwa tunayo sheria – sisi kama binadamu tunayo sheria iliyoandikwa mioyoni mwetu inayohitaji kifo ili msamaha kutekelezwa.

> Lakini ninaona kuna sheria nyingine inayotenda kazi katika viungo vya mwili wangu inayopigana vita dhidi ya ile sheria ya akili yangu.Sheria hii inanifanya mateka wa ile sheria ya dhambi inayofanya kazi katika viungo vya mwili wangu. (24) Ole wangu, mimi maskini! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Warumi 7:23-24

Unaweza kuwa huru kutoka kwa sheria hii ya kifo? Unaweza kuwa huru kutoka kwa mfumo wa haki ambao hutaka kufa kwa waovu? Mtazame Yesu msalabani na uone thamani ya fidia ambayo sote tunaelewa ilihitajika ili haki kuridhishwa. Ni haki ya Shetani ililidhishwa Msalabani kwa sababu alikuwa mtekaji nyara ambaye aliiba mioyo ya wana wa Mungu na kudai fidia. Sisi kama waliotekwa nyara njia pekee kwetu kuwa huru ilikuwa kulipa fidia ya kifo. Mungu hakuweka thamani ya fidia, Shetani aliweka.

# 7. Kama vile Musa alivyomwinua yule Nyoka kule Jangwani

Katika mfumo kwamba Yesu alikufa kuridhisha wazo la Shetani la haki ili jamii ya mwanadamu kukubali kwamba Mungu anaweza wasamehe sasa tuko tayari kuchunguza kwa ukaribu maneno ya Yesu kuhusiana na nyoka mtini.

> Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka kule jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa juu, Yohana 3:14

Kwa wanafunzi wengi wa Bibilia usambamba kati ya Yesu kuwekwa msalabani na nyoka aliyeinuliwa juu ya mti unaoneka kuwa ajabu kabisa. Haya mawili yanahusiana vipi?

> Wakasafiri kutoka mlima wa Hori kwa njia ya Bahari ya Shamu; ili kuizunguka nchi ya Edomu, watu wakafa moyo kwa sababu ya ile njia. (5) **Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani?** Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu. (6) **Bwana akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa.** (7) Watu wakamwendea Musa, wakasema, **Tumefanya dhambi kwa sababu tumemnung'unikia**

> **Mungu, na wewe; utuombee kwa Bwana, atuondolee nyoka hawa**. Basi Musa akawaombea watu. (8) Bwana akamwambia Musa**, Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi.** (9) Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti, **hata ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi**. Hesabu 21:4-9

Sababu ambayo ilipelekea uwepo wa nyoka ni kuwa kupitia kwa manugunika watu walibomoa ua wao wa ulinzi.

> Mwenye kuchimba shimo atatumbukia ndani yake; Na yeye abomoaye boma, nyoka atamwuma. Mhubiri 10:8

Wale ambao wanamheshimu Mungu kwa kutunza sheria zake wanao ulinzi wa Malaika wake. Watu wanapoendelea kuvunja sheria zake malaika hawawezi kuwalinda watu kwa urahisi.

> Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa. Zaburi 34:7

> Kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima, Wote wafanyao hayo wana akili njema, Sifa zake zakaa milele. Zaburi 111:10

Mungu hakuwatuma nyoka bali aliwaruhusu waje kwa sababu malaika wake hawakuwa na uwezo wa kuendelea kuwalinda kwa sababu walivunja sheria zake. Lakini watu walidhani kuwa ni Mungu aliyewatuma nyoka. Ufahamu wao wa haki ni kuwa uovu lazima uadhibiwe. Hivyo walidhani kwamba Mungu alihusika kikamilifu kuwaua watu kwa sababu ya dhambi zao. Musa aliagizwa kutengeneza nyoka wa shaba. Chuma hiki ni muhimu kwa sababu sio chuma ambayo inapatikana kiasili ardhini. Ni mchanganyiko wa vyuma viwili ambavyo Mungu aliumba navyo ni shaba nyekundu na zinki. Ni mmoja wa wana wa Kaini aliyetengeneza shaba.

> Sila naye akamzaa Tubal-kaini, mfua kila chombo cha kukatia, cha shaba na cha chuma; na umbu lake Tubal-kaini alikuwa Naama. Mwanzo 4:22

Shaba ni chuma iliyotengenezwa kwa mkono wa mwanadamu kutoka kwa vitu ambavyo Mungu aliumba na kuviunganisha pamoja. Shaba ni chuma ambayo wakati mwingine ina maana hasi katika Maandiko. Katika orodha ya laana za kutotii Bibilia inataja hii:

> Na mbingu zako zilizo juu ya kichwa chako zitakuwa shaba, na nchi iliyo chini yako itakuwa chuma. Kumbukumbu 28:23

Baada ya kuorodhesha uasi wa wana wa Israeli na uhalifu wao wa sheria, anawaambia:

> **Mwanadamu, nyumba ya Israeli imekuwa taka za fedha kwangu; wote wamekuwa shaba**, na bati, na chuma, na risasi, kati ya tanuu; wamekuwa taka za fedha. Ezekieli 22:18

Nyoka aliyetengenezwa kwa shaba aliwakilisha haki ya nyoka aliyetengenezwa kwa mikono ya mwanadamu. Nyoka ni mfano wa Shetani.

> **Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani,** aupotoshaye ulimwenguni wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake. Ufunuo 12:9

Baada ya baadhi ya Waisraeli kuuawa na nyoka na kutubu juu ya manuguniko yao walikuwa na imani kwamba dhambi ilikuwa imekabiliwa. Walitambua nyoka aliyeinuliwa kama mwangamizi wao wa dhambi. Wale ambao waliuawa walikuwa kafara ya dhambi. Kupitia kwa wazo hili la kuumbwa la mtu au shaba, Mungu aliweza kuwafundisha kwamba wanaweza pokea msamaha kwa ajili ya dhambi zao na kwa hivyo kuponywa. Hawangeweza kufahamu kuwa wazo lao la haki lilitoka kwa Shetani, hivyo Mungu alitumia wazo lao la haki na kuwaongoza kwa kutubu na uponyaji.

Katika njia sawa, Kristo aliinuliwa kusalimishwa kwa haki ya nyoka ili tuweze kuutazama msalaba na tuamini kwamba tunaweza samehewe. Ni kupitia kwa kifo cha Mwana wa Mungu pekee ndio sisi kama jamii ya wanadamu

tunaweza amini kwamba Mungu anaweza tusamehe na kwa hivyo hii ndio bei ya fidia ya kuweka akili zetu huru.

Katika hali yetu asili, yesu alitupa upatanisho badala wa dhambi zetu. Upatanisho huu unawakilishwa na nyoka wa shaba kwa sababu hiyo ndio bei ya mtekaji nyara kwa uhuru wetu. Ni uridhisho wa haki ya nyoka na ushahidi wake wa shaba. Sio ya uumbaji wa mbinguni mbali ya uumbaji wa mwanadamu na ya kizazi cha Kaini hasa.

Katika sura hii unapewa mtazamo mpya kabisa wa kuelwa mbona lazima Kristo angekufa kwa ajili ya dhambi zetu. Kanisa la Kikristo ni shupavu kwamba Mungu alihitaji kifo cha Mwanawe kwa wokovu wetu. Ila Bibilia inaelezea wazi.

> Dhabihu na matoleo hukupendezwa nazo, Masikio yangu umeyazibua, Kafara na sadaka za dhambi hukuzitaka. Zaburi 40:6

Mungu hakuhitaji kifo hiki lakini alijua kwamba mara tutakapoanguka mikononi mwa Shetani hawezi tuthibitishia kuwa anaweza samehe isipokuwa Mwanawe afe kwa niaba yetu.

Kama Mungu alihitaji Kifo cha Mwanawe basi kutolewa kwa dhabihu kungeadhimishwa katika ibada ya Mungu milele. Lakini kilichokinyume kabisa kilitendeka. Kupitia kwa kifo cha Kristo kanuni nzima ya kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi ilikoma.

> Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo **ataikomesha sadaka na dhabihu.** Dan 9:27a

Kristo angekomesha sadaka na dhabihu. Kristo aliinuliwa juu na aliwavuta watu wote kwake (Yohana 12:32). Mara tu mfumo wa shaba unaporidhishwa na tuukubali msamaha tunaweza pokea Roho wa Mungu kuwa nasi na mawazo yetu yabadilishwe. Hatuko chini ya mkuu wa shule

kamwe. Mara tu mawazo yetu yanapobadilishwa kamwe hatuhitaji kuupiga mwamba lakini kuunenea tu.

> “Twaa ile fimbo, ukawakusanye mkutano, wewe na Haruni ndugu yako, **ukauambie mwamba mbele ya macho yao utoe maji yake,** nawe utawatokezea maji katika mwamba, na hivyo utawanywesha maji mkutano na wanyama wao." Hesabu 20:8

La kuhuzunisha ni kwamba Musa hakufuata maelezo ya Mungu na kuuzungumzia mwamba. Manuguniko ya watu yalimkasirisha na kuonyesha mfano wa dhabihu katika kuupiga mwamba na kwa hivyo kuendeleza uelewa wa uongo wa haki na jinsi inaridhishwa. Hii ndio maana Mungu alirusuhu Musa kufa kabla ya kwenda mbinguni. Lazima watu wangeona kuwa wazo hili sio sahihi. Walihitaji kuona kuwa Mungu alihitaji wazungumze naye na kumuomba msamaha bila chochote kugongwa.

Udhaifu huu kwa upande wa mwanadamu haugeuzi mpangilio wa Mungu. Kwa hakika hutenda kazi na mfumo wetu wa haki ili kutuleta kwa Kristo. katika mfumo wa mwamba uliopigwa Mungu hutuvuta kuamini kwamba tumesamehewa na kisha maji ya uzima hububujika huru kutoka kwa Mwamba, Kristo Yesu.

> Na wote wakanywa kile kinywaji cha roho, kwa maana walikunywa kutoka katika ule mwamba wa roho uliofuatana nao, ule mwamba ulikuwa Kristo.
> 1 Wakorintho 10:4

> Hivyo, sheria ilikuwa kiongozi kutufikisha kwa Kristo, ili tupate tuhesabiwa haki kwa imani. (25) Lakini sasa kwa kuwa ile imani imekuja, hatusimamiwi tena na sheria. Wagalatia 3:24-25

Huduma aliyopewa musa kwa watu wenye shingo ngumu ilikuwa kukuza uovu wa mwanadamu katika kioo cha sheria ya Mungu.

> Basi ikiwa ile huduma iliyoleta mauti, ile iliyoandikwa kwa herufi juu ya jiwe ilikuja kwa utukufu hata ikawa Waisraeli

> hawawezi kuutazama uso wa Musa kwa sababu ya ule utukufu wake, ingawa ulikuwa ni wa kufifia: 2 Wakorintho 3:7

Ni jambo takatifu mtu kuona uovu wake mwenyewe. Mtu asili amepofushwa kuona uovu wake mwenyewe lakini sheria iliyotolewa kupitia kwa musa inatugutusha kwa hitaji letu kuu la injili ndani ya Kristo. Ni kioo hiki ambacho kimebarikiwa ndicho hutambua hali yetu potovu. Bila kioo hiki hatuwezi okolewa kwa sababu hatuwezi jua hali yetu ya hatari.

> Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa, lakini neema na kweli imekuja kupitia Yesu Kristo. Yohana 1:17

Bila shaka neema ya Yesu imekuweko tangu kabla ya kuweka msingi wa ulimwengu na leo bado tunahitaji kioo hiki katika sheria kutufundisha hali yetu potovu.

> Ambaye alituokoa na kutuita katika mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu mema bali **kwa sababu ya kusudi Lake mwenyewe na neema Yake. Neema hii tulipewa katika Kristo Yesu kabla ya kuwako kwa ulimwengu.** 2 Timotheo 1:9

Sheria na Injili zimetenda kazi pamoja tangu mwanzo wa anguko la mwanadamu mpaka sasa. Vyote vinahitajika kurejesha mwanadamu kukamilisha uhusiano na Mungu.


Kisa cha nyoka wa shaba ni muhimu kwa sababu nyingi. Kinatudhihirishia kwamba Kristo aliinuliwa juu ili kulipa hitaji la kanuni ya haki iliyoanzishwa na Shetani na kukumbatiwa na mwanadamu. Wakati uo huo tunapotazama nyuma Shaba kupitia kwa patakatifu kwa msingi wa Ibada ya Waisraeli tunatambua ushahidi zaidi kwamba Baba yetu mpendwa hakutaka Mwanawe afe lakini badala yake akamtoa kwetu ili tuweze kuamini.

> Ikiwa Mungu hakumhurumia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja Naye? Warumi 8:32

## 8. Ee Mungu Njia yako i katika Patakatifu

Kama mtoto nakumbuka nikitenda kazi ya kusoma Bibilia. Nilipofika katika kitabu cha kutoka nilipata mambo yakiwa magumu. Kusoma maagizo yote ya ujenzi wa patakatifu pa Mungu ilikuwa kazi ya kuchosha zaidi kwa mtu wa miaka 12. Lakini katika maagizo haya kuna ukweli wa thamani ambao unaelezea injili kwetu. Kama tujuavyo picha huchora maneno elfu, hapa kuna baadhi ya picha za kutupa maelezo ya haraka kuhusu Patakatifu


Court and Sanctuary
The Door
The Altar
The Laver
Holy Place
Most Holy Place


The Sanctuary
First Veil
Holy Place
Most Holy Place
Candlesticks (Light of the World)
Ark of the Covenant
Shewbread (Bread of Life)

Inapendeza kutambua vyuma vilivyotumika kwa samani ya Patakatifu.

| Samani | Vyuma vilivyotumika | Eneo |
|---|---|---|
| Madhabahu | Shaba | Ua |
| Birika | Shaba | Ua |
| Kinara cha taa | Dhahabu | Patakatifu |
| Meza ya mikate ya Wonyesho | Dhahabu | patakatifu |
| Chetezo | Dhahabu | Patakatifu |
| Sanduku la Agano | Dhahabu | Patakatifu mno |

Kuta za Patakatifu ziliundwa kwa mbao za dhahabu ikishikanishwa kwa matako ya fedha.

> "Nawe fanya hizo mbao za maskani za mti wa mshita, zenye kusimama. (16) Kila ubao utakuwa na urefu wa dhiraa kumi, na upana wake kila ubao utakuwa dhiraa moja na nusu. (17) Kila ubao utakuwa na ndimi mbili, zenye kuunganywa huu na huu; ndivyo utakavyozifanya mbao zote za maskani. (18) Kisha ufanye zile mbao za maskani, mbao ishirini kwa upande wa kusini kuelekea kusini. (19) **Nawe ufanye matako arobaini ya fedha chini ya zile mbao ishirini,** matako mawili chini ya ubao mmoja, kupokea zile ndimi zake mbili, na matako mawili chini ya ubao mwingine kupokea zile ndimi zake mbili…. **Na hizo mbao utazifunika dhahabu, na pete zake za kutilia yale mataruma utazifanya za dhahabu;** na hayo mataruma utayafunika dhahabu. Kutoka 26:15-19,29

Mapazia yaliyotumika ndani ya Patakatifu yaliunganishwa pamoja kwa dhahabu. Wakati ambao mapazia ya nje ya Patakatifu yaliunganishwa kwa shaba.

> "Kisha fanya hiyo maskani iwe na mapazia kumi; ifanye ya nguo ya kitani nzuri ya kusokota, pamoja na nyuzi za rangi ya samawi, na ya zambarau, na nyekundu, pamoja na makerubi;

> kazi ya fundi stadi… (6) **Kisha ufanye vifungo hamsini vya dhahabu, na kuunganya hayo mapazia pamoja kwa vile vifungo**; na hiyo maskani itakuwa ni moja. Kutoka 26:1,6

> "Nawe fanya mapazia ya singa za mbuzi yawe hema juu ya maskani… (11) **Tena ufanye vifungo hamsini vya shaba, na kuvitia vile vifungo katika zile tanzi, na kuiunganya ile hema pamoja**, ili iwe hema moja. (12) Na kipande kile kilichosalia, kile kiangukacho, cha yale mapazia ya hema, ile nusu ya pazia iliyosalia, itaanguka huko upande wa nyuma wa maskani. Kutoka 26:7-12

Wale ambao wametakaswa na injili wanakuwa wameondolewa shaba yote katika tabia zao. Maneno yao ni maneno safi.

> Neno linenwalo wakati wa kufaa, Ni **kama machungwa katika vyano vya fedha.** (12) Kipuli cha dhahabu, na pambo la dhahabu safi; Ndivyo alivyo mwonyaji mwenye hekima kwa sikio lisikialo. Methali 25:11-12

Mapazia ya nje ya Patakatifu ambayo bado ni ya shaba yanawakilisha miili yetu. Nyuzi hizi za shaba zitasafishwa wakati wa marejeo ya pili wakati miili yetu ya kufa itavishwa kutokufa.

> Sikilizeni, nawaambia siri: Sote hatutalala, lakini sote tutabadilishwa (52) ghafla, kufumba na kufumbua, parapanda ya mwisho itakapolia. Kwa kuwa parapanda italia, nao wafu watafufuliwa na miili isiyoharibika, nasi tutabadilishwa. (53) **Kwa maana mwili huu wa kuharibika lazima uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa lazima uvae kutokufa**. 1 Wakorintho 15:51-53

Mji wa mbinguni utajengwa kwa dhahabu safi ambayo ni kiwakilishi cha tabia ya wale ambao wanaishi pale.

> Ukuta huo ulijengwa kwa yaspi **hali mji wenyewe ulijengwa kwa dhahabu safi, iking'aa kama kioo**. Ufunuo 21:18

> Kwa hiyo nakushauri ununue kutoka Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto ili upate kuwa tajiri; Ufunuo 3:18

Kama tulivyogundua katika sura iliyopita, shaba ni tokeo la mwanadamu (Mwanzo 4:22). Inawakilisha jaribio la kuunganisha pamoja vitu vya Mungu kulingana na mawazo ya mwanadamu. Njia ya Mungu i katika patakatifu. Tunapoendelea kutoka kwenye ua hadi patakatifu mno, Shaba inasafishwa na dhahabu na fedha tu zinasalia. Tunapoendelea katika safari ya ukristo tunapaswa kuacha ua nyuma kwa sababu unaachiwa watu wa mataifa.

> Ndipo nikapewa mwanzi wa kupimia ulio kama fimbo, nikaambiwa, "Nenda ukapime Hekalu la Mungu pamoja na madhabahu, nawe uwahesabu wale waabuduo humo. 2) **Lakini usiupime ua wa nje wa Hekalu, uache, kwa sababu ua huo wamepewa watu Mataifa**. Hao wataukanyagakanyaga mji mtakatifu kwa muda wa miezi arobaini na miwili. Ufunuo11:1-2

Ua ni kwa ajili ya watu wa mataifa. Ni pahali ambapo wenye dhambi waliochafuliwa na mawazo ya shaba wanakutana na injili mwanzo. Madhabahu ya kafara yanawakilisha msalaba wa Yesu. Msalaba unawakilishwa na chuma shaba. Hivyo basi ni chombo kilichotengenezwa na mwanadamu, ni kitu ambacho mwanadamu alihitaji ili kuridhisha kanuni yake ya haki. Baada ya kukutana na Msalaba Mungu husababisha dhambi zetu kuwa nyingi katika kioo kinachopatikana katika birika ya shaba.

> Kisha akafanya hilo birika la shaba, na tako lake la shaba; **shaba hiyo ilikuwa ni ya vioo** vya wanawake wenye kutumika, waliokuwa wakitumika mlangoni mwa hema ya kukutania. Kutoka 38:8

Watu wanapojiangalia katika nuru ya sheria hisia zao za hukumu huongezeka hadi kwa kiwango ambacho wanakata tamaa ya maisha yao. Roho wa Kristo anapoingia ndani tunatiwa hatiani na dhambi.

> Naye atakapokuja, **atauthibitishia ulimwengu kuhusu dhambi**, haki na hukumu: Yohana 16:8

Kwa wale ambao kwa kweli wanaamini Mungu huwasamehe wanapotazama fidia katika hali yao ya kukata tamaa wakiwa wamesimama kando ya madhabahu ya kafara, neema huongezeka kwao, na huanza kupokea dhahabu ambayo ni imani ya kweli katika nafsi na hununuliwa katika tanuru ya mateso.

> Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi, Warumi 5:20

Kadri dhahabu ya imani yetu inaongezeka, ndivyo Shaba ya mawazo yetu ya kale inasafishwa hadi hatimaye hatuna utambuzi wa dhambi tena.

> Kama dhabihu hizo zingeweza kuwakamilisha, hazingeendelea kutolewa tena, kwa kuwa hao waabuduo wangekuwa wametakaswa mara moja tu, **wala wasingejiona tena kuwa na dhambi.** Waebrania 10:2

Kisha hakuna wazo tena la kutoa kafara, hakuna kuugonga Mwamba tena ila tu kunena na Mwamba.

> Lakini zile dhabihu zilikuwa ukumbusho wa dhambi kila mwaka, (4) **kwa sababu haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi**. (5) Kwa hiyo, Kristo alipokuja duniani alisema, "**Dhabihu na sadaka hukuzitaka,** bali mwili uliniandalia, (6) **sadaka za kuteketezwa na za dhambi hukupendezwa nazo.** (7) Ndipo niliposema, 'Tazama niko hapa, kama nilivyoandikiwa katika kitabu, Nimekuja kufanya mapenzi Yako, Ee Mungu.' (8) Kwanza alisema, "Dhabihu na sadaka, sadaka za kuteketezwa na za dhambi hukuzitaka, **wala hukupendezwa nazo" (ingawa sheria iliagiza zitolewe).** (9) **Kisha akasema "Tazama niko hapa, nimekuja kuyafanya mapenzi Yako." Aondoa lile agano la kwanza ili kuimarisha la pili.** (10) Katika mapenzi hayo sisi tumetakaswa na

> kufanywa watakatifu kwa njia ya sadaka ya mwili wa Yesu Kristo alioutoa mara moja tu. Waebrania 10:3-10

Yesu alikufa mara moja kwa ajili ya wote kama inavyowakilishwa na nyoka wa shaba juu ya madhabahu ya shaba. Lakini tunapojazwa Roho Msalaba huchukua mtazamo tofauti kabisa. Mkazo na kujikana nafsi kwa kupendeza kwa Kristo na Ufunuo wa tabia ya Baba katika Yeye. Madhabahu ya kafara (kuupiga Mwamba) yanabadilishwa na madhabahu ya chetezo (Kunena kwa Mwamba) – kumwagika kwa damu Kalvari kunaletwa katika muktadha wakumwagika kwa damu Gethsemane ambapo Yesu aliitimiza kazi aliyopewa na Baba yake.

> Yohana 17:4 Nimekutukuza Wewe duniani kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye.

Tazama juu na utaishi mdhambi mpendwa, Mungu hakumtuma Mwanawe ulimwenguni ili ahukumu ulimwengu (Yohana 3:16-17). Ndani ya utenda kazi wa madhabahu ya dhahabu Mungu alimtuma Mwanawe kudhihirisha tabia yake na kuibeba hatia yetu juu yake yeye mwenyewe ili tuweze kuamini katika msamaha wa Mungu.

Baba yetu mpendwa hakumtuma Mwanawe ili kutwambia kwamba "hivi ndivyo ningewatendea kwa sababu ya dhambi zenu lakini nikaamua kumuua mwanangu badala yenu katika hasira yangu." Ni Baba yupi anaweza tenda hili kwa wanawe? Uchunguze Msalaba tena kutoka kwa uwanja wa dhahabu na uone kitu cha thamani kwamba utalia kwa furaha.

Unapotoka kwenye ua la shaba na kuingia katika patakatifu pa dhahabu na fedha utaona kwamba haki ya Mungu ni tofauti kabisa na ya mwanadamu. Tunaambiwa.

> Tazama, utaita taifa usilolijua, na taifa lisilokujua wewe litakukimbilia, kwa sababu ya Bwana, Mungu wako, na kwa ajili yake Mtakatifu wa Israeli; maana amekutukuza. (6) Mtafuteni Bwana, maadamu anapatikana, Mwiteni, maadamu yu karibu; (7) Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki

aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, **Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa**. (8) **Maana mawazo yangu si mawazo yenu,** wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. (9) **Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.** (10) Maana kama vile mvua ishukavyo, na theluji, kutoka mbinguni, wala hairudi huko; bali huinywesha ardhi, na kuizalisha na kuichipuza, ikampa mtu apandaye mbegu, na mtu alaye chakula; (11) ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma. (12) **Maana mtatoka kwa furaha, Mtaongozwa kwa amani; Mbele yenu milima na vilima vitatoa nyimbo; Na miti yote ya kondeni itapiga makofi**. (13) Badala ya michongoma utamea msunobari, Na badala ya mibigili, mhadesi; **Jambo hili litakuwa la kumpatia Bwana jina, Litakuwa ishara ya milele isiyokatiliwa mbali.** Isaya 55:7-13

Ni ombi langu la kipekee kwamba utauona Msalaba wa Yesu kwa mtazmo mpana wa mwanga mzuri uliosafishwa haki ya shaba ya watu walioanguka na malaika walioasi. Kuja kwa nuru tamu ya Upendo wa Baba ambapo Agape yake inauwezo wa kuondoa hofu yote.

Katika neema ya Yesu,
nimeokolewa
Nilipotea dhambini,
Nilikuwa kipofu rohoni

Bali neema ya Yesu
Yanitosha sana
Ilinifungua macho yangu,
Ikanifungua

Nilikuwa mwenye hofu
Nilifungwa nazo.
Nimefunguliwa sasa

Kwa neema ya Yesu

Katika neema ya Yesu,
nimeokolewa
Nilipotea dhambini,
Nilikuwa kipofu rohoni

# 9. Sela

Kwa Mkombozi wangu mpendwa, ulinijia katika giza la dhambi. Ulinihakikishia msamaha wa Baba kwa njia ambayo singeweza kufahamu na kukubali. Nalia kwa sababu ya uchungu ulioteseka kwa ajili yangu. Ukiwa umejawa na huruma ya Baba yako ulivumilia usiku wa giza ya ulimwengu huu kuwaokoa kondoo wako masikini waliopotea.

Ni jinsi gani moyo ulivyo polepole kufahamu uhalisia wa yale umetenda. Umilele hauwezi nidhihirishia kina cha upendo wako. Ni chemchemi isiyokauka ambayo kwayo nitakunywa milele na kamwe sitachoshwa na ladha yake.

Ni hamu yangu kukufuata, mwana-kondoo wa thamani, popote uendako. Umenunua kwa gharama isiyohesabika. Ingawa wakati mwingine nahisi nisiyestahili upendo wako, naamini hautaniacha kamwe wala kuniondokea. Nashukuru kwa kunitumia roho wako wa thamani kunifariji na kunibariki.

Mkombozi mpendwa ninahamu kuu zaidi kuwa wale ambao umenipa katika ujumbe huu pia wawe nasi katika ufalme wa Baba. Nahisi upendo wako moyoni mwangu na hamu yangu ni kuu kwa ukombozi wao. Nakushukuru kwamba naweza onja upendo wako kwa wana wako na kuunganika nawe katika mapenzi yako kwa ulimwengu kumjua Baba yetu kwa kweli.

Ni ruzuku Roho wako mtamu ili niweze kukutukuza kama ulivyomtukuza Baba vizuri kwa ajili yetu. Naomba udhihirishwe kwetu katika miili yetu ili kwamba mioyo ya watu iweze kupokea upatanisho kwa maana umetuamuru tutende kazi ya maridhiano.


Ruzuku kila mmoja asomae kitabu hiki dawa ya macho ili kuona uzuri wa kweli wa msalaba na kwamba sisi sote tukome kuhofu kusulubiwa nawe kwamba kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri kuwa wewe ni Bwana kwa utukufu wa Baba yetu mpendwa.

Katika jina lako la thamani Bwana Yesu

Amina.

Vitabu vingine vinapatikana katika fatheroflove.info
pia kuna vitabu vyenye sauti kwa kushushwa bila malipo

## Agape





Chukua mtazamo wa kina katika ushahidi wa Bibilia kuwa Mungu wa Agano la Kale ni sawa na kile ambacho Yesu alidhihirisha katika Agano Jipya. Kitabu ni maelezo ya ndani na majaribu taratibu ya kweli ambazo zinatupa njia ya moja kwa moja ya kutazama hadithi kadhaa za Bibilia ambazo hazijaangaziwa hapo awali. Kwa kurasa 300 tu, huu ni mfululizo wa somo kwa wale ambao wanatafuta majibu kweli. Wema Mkuu kwa kijitabu hiki unao mikononi mwako.

## Upendo Asili




Ndoa kama taasisi iko katika tishio kubwa. Mbona watu wengi zaidi wanaushuhuda mbaya wa ndoa na uhusiano kwa jumla? Upendo asili hutafuta uhusiano asili unaoelezewa katika Bibilia kuona vitu ambavyo tunaweza jifunza kuwa uhusiano wetu wenyewe unaweza imarishwa na kuboreshwa. Kurasa 44 zikipakiwa na kanuni muhimu za ndoa mahiri.

## Vita vya Utambulisho




Vita vya utambulisho ni safari ya kujitambua binafsi. Ni makaribisho ya kujifunza kuhusu thamani yako katika muktadha wa mahusiano. Kitabu hiki kinadhihirisha kanuni ambazo zitakusaidia kuepuka matendo yanayoongozwa na mawazo ya ulimwengu huu na kupata uhuru katika uhusiano wako muhimu zaidi.

# Msalaba uliotahiniwa

# &

# Msalaba Ulioshuhudiwa

Mbona msalaba ulihitajika na nani aliuhitaji?

Mbona msalaba ulikuwa muhimu kwa ukombozi wetu?

Je, ghadhabu ya Mungu iliridhishwa na kifo cha Mwanawe?

Haki ya Mungu ni nini na ina tofauti na haki yetu?

Mbona Yesu alijilinganisha na Nyoka wa shaba juu ya mti?

Patakati pa Waisraeli panatwambia nini kuhusiana na Msalaba?